ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa
11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa

12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu
22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka

23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
34.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
35. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
36.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
38.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake

40.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
42.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
43.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
44.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
45.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
46.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
47.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
48.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
49.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
50.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
51.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
53.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
54.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
55.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
57.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
58. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
59.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
60.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
61.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

62.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
63.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
65.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
66.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
67.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
68.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
69.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
71.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
72.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Yahya Khamis Hamad **Kny:Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Saba – Tarehe 26 Januari, 2012

Kikao Kitaanza Saa 3:00 Asubuhi

DUA

Mhe. Spika, (Pandu Ameir Kificho) alisoma Juma

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Mindombinu na Mawasiliano naomba kuweka hati ya kuwasilisha Mezani Kusiana na taarifa rasmi kuhusu hitilafu za kiufundi kwa vyombo vya baharini, siku za hivi karibuni.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Rashid Seif Suleiman Kny/ Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujezi: Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza la Wawakilishi naomba nihudhurishe Mezani maoni ya Kamati kuhusu ripoti ya Mhe. Waziri.

Naomba kuwasilisha.

TAARIFA

Mhe. Spika: Waheshimiwa kabla ya kuanza masuali naona kuna taarifa ya wageni. Waheshimiwa Wajumbe kama ilivyo kawaida Baraza letu huwa linatembelewa na wageni mbali mbali ili wafarijike kuona namna ya shughuli zetu zinavyoendelea.

Leo hii katika ukumbi wetu wa juu kuna wageni ambao ni serikali ya wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Elimu Chukwani naomba tuwatambue na niwaombe ndugu zetu, vijana wetu hao wote wasime kwa pamoja ili kupokelewe na Waheshimiwa Wajumbe.

Karibuni sana ili muone wazee wenu namna wanavyoendesha shughuli, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko humu ndani. Sasa mmebahatika leo kuzungumza Waheshimiwa Wajumbe na Serikali ya Wanafunzi na *counter party* wenu kwa chuo cha Chukwani. Karibuni sana.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 41

Migogoro ya Ardhi

Mhe. Jaku Hashim Ayoub Kny/Mhe. Hamza Hassan Juma: Aliuliza:-

Hivi sasa hapa Zanzibar kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi na Wizara yako imekiri kupitia kwenye hotuba zako mbali mbali. Hata na Mhe. Rais amekuwa akilielezea katika hotuba zake mbali mbali, ikiwemo uvamizi wa ardhi za watu, mashamba ya watu na kadhalika.

(a) Je, Mhe. Waziri Serikali imelichukulia uzito kiasi gani suala hilo.

(b) Je, Wizara yako imepokea malalamiko mangapi hadi sasa na mangapi imeyachukulia hatua.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Makamo wa Pili wa Rais naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi, suala lake Nam 41 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:

(a) Ni kweli nchi yetu inakabiliwa na migogoro ya ardhi hasa wakati huu ambapo Sekta ya Utalii inazidi kuimarika. Serikali kupitia Wizara ya Ardhi Makaazi, Maji na Nishati inalishughulikia suala hili ili kutapa ufumbuzi muafaka utakaoondoa migogo hiyo na tayari hatua mbali mbali zimechukuliwa, na miongoni mwa hatua hizo ni kama zifuatazo.

i) Kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi katika ngazi za mikoa, Wilaya ya Vijiji ili kuweka bayana ardhi iliyopo na matumizi yake.

ii) Kuandaa sera mpya ya ardhi ambayo itaweka misingi imara na madhubuti zaidi kwa serikali na kwa wadau wote wa ardhi juu ya umiliki, matumizi na usimamizi wa ardhi ya Zanzibar.

iii) Kuzifanyia mapitio sheria saba za ardhi kwa lengo la kuimarisha utekelezaji na usimamizi wake ili kuondoa migogoro mbali mbali ya ardhi.

iv) Kufanyia mapatio mpango mkuu wa Mji wa Zanzibar wa mwaka 1982 ili ukidhi haja ya ongezeko la idadi ya watu na ukuaji wa miji na kuweka misingi imara inayoendana na mabadiliko ya mahitaji ya matumizi ya ardhi.

v) Kuendelea na utoaji elimu kwa wananchi juu ya masuala mbali mbali ya ardhi ili kuwajengea uelewa juu ya masuala hayo .

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu imepokea malalamiko yapatayo 107 ya ardhi, ambayo katika malalamiko hayo, malalamiko 27 kawa na 28.6% ndiyo yaliyokwisha kupatiwa ufumbuzi na yaliyobaki yanaendelea kushughulikiwa kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Aidha SMZ inawaomba wananchi kufuata sheria na taratibu za ardhi zilizopo ili kuepuka kujiingiza katika migogoro isiyo ya lazima.

Mhe. Spika, natoa wito kwa viongozi wa Shehia, Halmashauri za Wilaya na Mikoa na wale wote wasiohusika na mambo ya ardhi waache mara moja kujiingiza katika masuala hayo. Kwani kufanya hivyo ndio inakuwa chanzo cha migogoro hii kutokana na tamaa zao binafsi, jambo ambalo serikali haitolivumilia.

Mhe. Spika, naomba nitanabahishe kuwa Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati, pekee ndiyo yenye mamlaka ya kisheria ya ugawaji wa ardhi nchini.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsate sana Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ya ufasaha kabisa. Vile vile niipongeze Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa kushughulikia matatizo na migogoro ya Ardhi. Pamoja na maelezo mazuri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

(a) Mhe. Spika, sheria inafanyiwa marekebisho muda mrefu, kuchelewa kuanzia Mahakama za Mikoa, huoni ni kucheleweshaha haki za wananchi.

(b) Kati ya malalamiko haya ya migogoro ni mingapi inayohusu vigogo au viongozi na ni akina nani?

(c) Kwa sababu serikali inakiri kwamba kuna migogoro mingi haioni kwamba wakati umefika wa kuunda tume ya Kitaifa kuchunguza migogoro hiyo ya ardhi ili kuzingatia misingi ya utawala bora.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mh. Spika, naomba kujibu kwa pamoja. Mhe. Spika, utaratibu wowote wa kutunga sheria unafuata taratibu zilizowekwa. Lakini pia inakwenda kutokana na mahitaji halisi. Hivi sasa hatua mbali mbali zinachukuliwa ili Mahakama ya Ardhi iweze kufanya kazi zake vizuri, ikiwa ni pamoja na kuteuwa Mahakimu katika Mikoa yote mitano kwa ajili ya kushughulikia kesi hizi za masuala ya ardhi. Na mambo mengine yanayochukuliwa kubadilisha sheria Mhe. Spika, ni ya kitaalamu, kwa hivyo si kuchelewa isipokuwa nia yetu ni kuweka mazingira mazuri ya kutatua matatizo yaliyopo.

Mhe. Spika, kuhusika kwa viongozi kutokana na migogora hii ya Ardhi. Viongozi kama binaadamu wengine hutokea kufanya makosa. Kwa hivyo wapo viongozi mbali mbali katika ngazi za Shehia, Mikoa, Wilaya na hata katika ngazi ya Kitaifa wanaotokea kujihusisha na utaratibu huu wa migogoro ya ardhi. Jambo ambalo kama nilivyosema katika suala la msingi serikali kwa sasa haitolivumilia na mtu yeyote atakaye shirikia kinyume na utaratibu uliowekwa hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Mhe. Asha Bakar Makame: Ahasante sana Mhe. Spika, kwa kunipatia fursa hii ya kuuliza suala la nyongeza kama hivi ifuatavyo:-

Kwa kuwa huko nyuma kulikuwa na malalamiko mbali mbali ya uvamiaji wa ardhi. Na kwa kwa kuwa majibu ya Mhe. Waziri aliyojibu ni kutengenezwa sera maalum. Je, haoni kama kuna haja sasa hivi ya kufanya utafiti wa kina kwa kila Mkoa ili kuhakikisha ardhi imevamiwa namna gani na ni nani na nani waliovamia ardhi hiyo, kama ni Masheha, kama ni Wakuu wa Mikoa, kama ni Wakuu wa Wilaya au Viongozi wa Kitaifa.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, ushauri wa Mhe. Asha Bakari Makame ni mzuri na ndio tunaoufanyia kazi kwa sasa. Wizara inayosimamia mambo ya Ardhi inafanya utafiti huo kuona kila ambapo pametokea makosa parekebishwe. Ndio maana ikaja mapendekezo haya mbali mbali kwa niya hiyo ya kuondoa migogoro iliyopo. Lakini hata hivyo kama nilivyosema awali hatua kali zitachukuliwa kwa wale wote watakaovunja utaratibu na kutoa ardhi bila ya kufuata taratibu zilizowekwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza suala dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Waziri umekiri kwamba wanaosababisha matatizo haya ya ardhi mara nyingi ni viongozi wa Shehia, Wilaya pamoja na Mikoa. Lakini vile vile na upande mmoja na taasisi za serikali zinahusika kwa kiasi kikubwa katika kusababisha matatizo ya ardhi.

(a) Je, ni lini serikali itawalipa fidia wakulima ambao imetumiwa ardhi yao kwa ajili ya kujenga majengo ya serikali kama vile Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichopo pale Vitongoji.

(b) Kwa kuwa wananchi katika vijiji mbali mbali kikiwemo kijiji Vitongoji katika jimbo la Wawi, wana uhakika kwamba kuna baadhi ya viongozi wakiwemo Masheha pamoja na Viongozi wa Wilaya na wanawajua kwa majina, ndio wanaosababisha kuchukua ardhi yao na kuwakabidhi matajiri pamoja na viongozi wengine wa Serikali.

(c) Je, ni lini serikali itawasaidia wananchi wale kuwapatia uwezo wa kuwapeleka katika vyombo vya sheria kusudi haki yao iweze kupatikana.

(d) Je. Kuendelea kuwadharau wakulima wale wa Vitongoji katika eneo la ardhi yao na kuwakabishi matajiri, si kwenda kinyume na haki za binaadamu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naomba kuendelea kumjibu muasisi mwenzangu masuala yake ya nyongeza yenye (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo.

(a) Kuhusu suala la fidia ni utaratibu uliowekwa kiserikali kwamba wale ambao wana milki zao na pale serikali inapotaka kuchukua mashamba hayo kwa ajili ya kufanya shughuli za maendeleo ya umma basi utaratibu unawekwa kwa kulipwa fidia wahusika hao. Nitachukua hatua ya kumtafuta Mhe. Saleh ili tuzungumze zaidi niweze kujua kwa undani wa fidia anayoizungumza kwa sababu kuna utata kidogo wa suala zima la fidia katika maeneo yale ya Fidel-Casro kule Pemba. Lakini tutazungumza na Mhe. Saleh ili tuweze kulimaliza tatizo hili.

(b) Mhe. Spika, Mheshimiwa amesema kwamba wapo viongozi wanaojiingiza katika masuala haya ya ugawaji wa ardhi na matokeo yake wanasababisha migogoro.

(c) Kama nilivyosema katika suala langu la msingi kwamba hao wanaofanya hivyo wanafanya kwa tama zao binafsi, sio kwa nia njema ya serikali ya kuondosha matatizo hayo. Hivyo tutashauriana na Mhe. Saleh ili viongozi hao walioshiriki katika kunyang'anya rasilimali za wananchi tuwafahamu na hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa.

Nam. 85

Kuzagaa kwa Vifaa Vilivyotumika "*USED*"

Mhe. Mussa Ali Hassan - Aliuliza:-

Baadhi ya wananchi wa Zanzibar wanajishughulisha na biashara ya uuzaji wa vifaa vilivyotumika maarufu "used". Baada ya vifaa hivyo kuuzwa vyengine hubakia na huwa havina matumizi tena.

(a) Kwa kuwa Zanzibar tuna Sheria ya Kuhifadhi Mazingira, na kwa kuwa wafanyabiashara huviwacha vifaa vinavyobakia kuzagaa ovyo. Je, Mhe. Waziri kitendo hicho cha kuviacha vifaa hivyo sio kwenda kinyume na sheria hiyo.

(b) Je, Mhe. Waziri, Serikali ina mpango gani kuhusiana na vifaa hivyo vinavyobakia.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko - Alijibu:-

Ahsante Mhe. Spika, kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 85 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, kuwacha vifaa vilivyobakia kutoka na uuzaji wa vifaa vya "Used" ambavyo vinaonekana havifai tena kuzagaa ovyo ni kinyume cha Sheria Nam. 2 ya 1996 ya Kusimamia Mazingira.

(d) Mhe. Spika, kwa vile suala hili linasimiwa na Sheria ya Kusimia Maszingira ni imani yangu kwamba wenzetu katika kitengo hichi cha mazinga kulingana na kanuni zao wana mpango madhubuti wa kulishughulikia suala hili. Sheria ya Wizara ya Biashara,Viwanda na Masoko ni ya kumlinda mtumiaji.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Ahsante Mhe. Naibu Waziri kwa majibu ambayo umenijibu, lakini nataka kujua ni wafanyabiashara wangapi wamechukuliwa hatua ama kushtakiwa kutokana na uharibifu huu wa mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza ya Rais: Nakushukuru Mhe. Spika, naomba kuongeza majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko. Pia kutoa maelezo juu ya suala la ziada la Mhe. Mussa Ali Hassan kama ifuatavyo.

Mhe. Spika, kama alivyoongea Mhe. Naibu Waziri, Sheria ya Uhifadhi wa Mazingira Nam. 1996 inasimamiwa na Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais. Tatizo hilo ni kama changamoto ambayo tumekuwa tunaiongea kwa muda mrefu hapa visiwani kwetu. Suala zima la uingizwaji wa vifaa chakavu yaani *used products* kutoka nchi mbali mbali za Ulaya na sehemu nyengine za ulimwengu limekuwa ni tatizo kubwa.

Kama mtakumbuka Waheshimiwa Wajumbe juzi wakati tunaongea katika Semina juu ya kuzungumzia masuala mazima ya kubadilika kutoka kwenye mfumo wa analogi kwenda kwenye mfumo digital, tuliambiwa kwa vifaa vya televishen tu peke yake basi tayari zipo laki tatu ambazo hizo zitakuwa hazifai kwa kipindi hicho kama zitakuwa hazikuwekewa vifaa maalum. Ni changamoto ambayo vipi tutaziondosha, vipi tutaweza kuondoa uchafu huo.

Mhe. Spika, naomba niwaarifu waheshimiwa wajumbe kwamba ofisi yangu tayari imeshaandaa kanuni ambayo itasimamia uingizwaji wa bidhaa chakavu nchini, kwa madhumuni mazima ya kudhibiti nchi yetu isigeuzwe kuwa jaa la kutupa vifaa chakavu ambavyo huko kwao na baadhi ya nchi hata huko kwao wanavizuia visitoke kwenda kwenye nchi nyengine lakini kwa njia za panya vitu hivyo vinatoka na kuingia ndani ya visiwa vyetu.

Mhe. Spika, tatizo ya bidhaa chakavu ni kubwa na lina pande mbili na linahusisha wadau wengi, linahusisha Wizara ya Biashara kwa maana ya kulinda walaji. Linahusisha Afisi ya Rais na Baraza la Mapinduzi kwa maana ya kuweza kudhibiti uchafu wa takataka hizo. Lakini pia linahusisha Afisi yangu kwa maana ya suala zima la kuzuia uharibifu wa mazingira.

Changamoto iliyomo kwenye bidhaa chakavu ni mbali, kwanza tuna *material* kama vyuma ambavyo kama mafriji au televishen, vitu ambavyo vinaweza vikatumika tena, vile tunaweza tukavitumia. Lakini kibaya zaidi kuna takataka za sumu ndani ya vifaa hivi hasa vya *electronic* ambavyo vinaingizwa hapa, uharibifu wake kama visiwa kama Zanzibar, kwa kweli hatuna uwezo wala vifaa vya kuweza kuharibu, inabidi kama alivyozungumza Mhe. Waziri tushirikiane na wenzetu mataifa yanayotupa ushirikiano ili kuweza kuziondoa takataka hizo za sumu ndani ya visiwa vyetu. Iliwahi kufanyika hivyo miaka ya nyuma na tunajipanga kuona jinsi gani tunaweza tena kupata msaada huo, ili kuondosha takataka hizo. Nakushukuru.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya nimuulize suala dogo la nyongeza Mhe. Waziri. Mhe. Waziri alivyokuwa akijibu alisema kwamba Wizara inaandaa kanuni kwa ajili ya kushughulikia zoezi zima la mambo ya *used*. Nilikuwa nataka kujua sijui kanuni hizo zitakuwa lina tayari na zitaanza kutumika lini.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza ya Rais: Mhe. Spika, ni muhimu kanuni hizi kuwashirikisha wadau wote, suala la ushirikishwaji wa wadau katika masuala kama haya ni muhimu ili liweze kufanikiwa. Nimuahidi Mhe. Mwakilishi na Wajumbe wako wote kwamba haitazidi miezi miwili kanuni hii itakuwa tayari kwa kuweza kutumika.

Nam. 87

Barabara ya Mkunazini

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Barabara ya kutoka *Traffic Light* kwenda Mkunazini ni barabara ambayo ipo kwenye Kitovu cha Mji wa Zanzibar ni barabara muhimu mno kwa shughuli za kitalii.

(a) Je, Mhe. Waziri, wizara yako inajua kuwa ile barabara ni mbovu sana kiasi cha kusema haipitiki.

(b) Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza barabara hii ili kuhuisha haiba ya Mji wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na
Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 87 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, wizara yangu inafahamu kwamba barabara ya kutoka Mkunazini kuelekea *Suni School* ni mbovu, lakini sio katika kiwango cha kutoweza kupitika.

(b) Mhe. Spika, barabara hiyo imo katika mpango wetu wa kutaka kuijenga upya kwa kupitia fedha za mfuko wa barabara. Aidha, kupitia mfiko wa barabara tunafanya mapitio ya miradi na mategemeo yetu kwamba kwa kushirikiana na Manispaa na Idara yetu ya UUB, Mfuko wa barabara pamoja na mchango wa Mhe. Mbunge wa Mji Mkongwe matarajio yetu kwamba barabara hiyo itajengwa katika robo ya pili yaani kutoka April – June.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, juu ya majibu mazuri aliyetoa Mhe. Naibu Waziri,

(a) Je, kuna mpango gani wa dharura kwa vile wananchi wanaoishi katika Mji Mkongwe wamekuwa katika mazingira magumu yakurushiwa maji machafu kwenye nguo zao hasa siku ya Ijumaa mvua zinaponyesha, maji hutuama katika mashimo. Ukingatia mji Mkongwe una misikiti mitatu mikubwa ya suala la Ijumaa.

(b) Kwa vile barabara hiyo ni njia kuu ya watalii kwenda kwenye kumbukumbu la soko la watumwa na viongozi wa serikali kuja kuangalia. Serikali haiyoni kuna umuhimu wa kujenga barabara hiyo kabla ya mwakani, kwa kuzingatia utalii unachangia asilimia 25 pato la taifa.

(c) Mhe. Naibu Waziri kwa vile barabara hiyo kwa vile ilijengwa na mfanyabiashara maarufu almarhum Said Al –Batashi, je serikali ina mpango gani kuenzi mchango wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, tumeeleza kwamba kwa kushirikiana na mfuko wa barabara na wenzetu wa Manispaa na kwa kuthamini mchango wa Mhe. Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe tunarejea tena kufanya mapitio ya miradi. Madhumuni yetu kwamba katika robo ya kutoka April – June barabara hii itakuwa imejengwa. Tumuombe sana Mhe. Mwakilishi, avute subira, kipindi cha miezi mitatu kwa kusubiri mradi kama huu mzuri ambao utawaepusha watu kuchafua nguo zao, kuenzi ule mchango ambao umetolewa na yule aliyejenga mwanzo barabara ile bwana Batash.

Basi namuomba Mhe. Mwakishili afanye subira, asubiri hadi mwezi April kuelekea June barabara ile tutakuwa tumeshaijenga na tutaijenga kwa kiwango cha lami na itapendeza.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kuwa barabara za mjini zinashughulikiwa na vyombo viwili. Wizara hii ya Mawasiliano na Miundombinu na Manispaa. Hawaoni kwamba watatiwa aibu na Manispaa kwa kuwaendekeza katika utengenezaji wa barabara, kwani ule uchimbukaji wa eneo la daladala sasa unaingia barabarani kwa kudharauliwa kutengenezwa.

Kwa hivyo je, Wizara ya Mawasiliano kuliachia suala hili kwa manispaa peke yake, hawaoni kwamba wao watakuja kubeba mzigo baadaye.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kufafanua zaidi na kujibu suala la Mhe. Mwakilishi. Lakini pia kufafanua zaidi majibu ambayo Naibu Waziri amekuwa akiyatoa.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa kanuni barabara zote za Mjini ziko chini ya uangalizi na usimamizi wa Manispaa ya Zanzibar. Ni mara chache tu ambazo serikali kwa kupitia wizara inawasiliana na Manispaa katika barabara ambazo ni kubwa, lakini hizi ndogo ndogo kama hiyo ambayo inatoka Darajani kuelekea Mkunazini, inayotoka jumba Nam. 6 kupitia Mwembetanga mpaka Mchangani na nyenginezo hizo zote ziko chini ya Manispaa.

Mhe. Spika, Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe ambalo jimbo hilo lina barabara hizo kwa kutumia fedha za mfuko kutoka Bunge kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri amekubali milioni 20 kutumika kwa shughuli hiyo. Tumeshawasiliana na Manispaa pamoja na kwamba Manispaa na sisi ni serikali, lakini kila mtu ana mipaka yake na Manispaa kwa barua rasmi wamekubali kwamba tushughulike na kuzitengeneza barabara hizo kwa kutumia fedha hizo.

Kwa hivyo, kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba fedha zitatolewa wakati wote kuanzia sasa na ni kwa ajili ya mafuta kwa sababu vifaa tunavyo na baadhi ya *material* tunayo. Kwa hivyo, fedha hizo zaidi ni kwa ajili ya mafuta ya kuchukulia vifaa hivyo kutoka Kibele au popote kuvileta pale pamoja na lami.

Mhe. Spika, wakati najibu suala hili ni kwamba barabara zitakazotengenezwa kwa kutumia fedha hizo ni kutoka mwisho wa jumba Nam. 6 kwa kupitia Mwembetanga mpaka mahali ambapo njia inakutana na njia ya Mchangani. Tukitoka pale tunaelekea njia ya Vikokotoni mpaka Darajani tunakwenda zetu mpaka Donge ambapo sasa hivi kuna benki pale. Kwa hivyo, tunaamini kabisa kwamba barabara hiyo na nyengine ambayo ni kutoka *round about* au *traffic light* kuelekea kwa Batashi nazo hizo zote zitatengenezwa katika kipindi hiki.

Lakini kutokana na fedha za mfuko wa Jimbo la Mji Mkongwe ndio tumeweza, hizi hazimo kwenye bajeti ya serikali na ni mara nyengine tunawaomba watu wa mfuko, na watu wa mfuko na wao wanapokuwa wako tayari ndipo tutafanya barabara hizo Kwa hivyo, Mhe. Spika, si kwa sababu yote lakini kwa sababu barabara hizi kwanza ziko chini ya Manispaa, lakini vile vile Manispaa hawana fedha za kutosha kuweza kutengeneza na hata wakitaka kutengeneza wanatwambia sisi tutengeneze kwa gharama zao, lakini mara hii Mbunge wa Jimbo la Mji Mkongwe ameweza kulifanya hivyo.

Kwa hivyo, tunawaomba na Wabunge wengine na Wawakilishi wengine shughuli kama hizi wanazo fedha kidogo basi wasaidie Wizara ya Miundombinu kwa kutumia *UUB* angalau kwa mafuta kwa sababu vifaa tunavyo. Mhe. Spika, na hiyo milioni 20 ni asilimia 25 ya gharama ya matengenezo ya barabara zile kwa hivyo serikali pale kwa kutumia mfuko nayo

itachangia karibu asilimia 75 kwa njia ya mshahara, kwa njia ya mafuta na kwa njia ya vifaa. Mhe. Spika, nilitaka nilifafanue hili kwa Waheshimiwa Wawakilishi.

Nam. 82

Uanzishwaji wa Baraza la Taifa la Vijana

Mhe. Wanu Hafidh Ameir – Aliuliza:-

Katika Uzinduzi wa Baraza la Nane la Wawakilishi Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika hotuba yake aliahidi kukamilisha Uanzishaji wa Baraza la Taifa la Vijana ambalo litaimarisha ushiriki wa vijana katika ngazi mbali mbali za maamuzi na kupiga vita ukimwi na kuendeleza mapambano dhidi ya dawa za kulevya. Kwa kuwa hivi sasa vijana wengi wameathirika na dawa za kulevya lakini pia hivi sasa maambukizo ya ukimwi miongoni mwa vijana wenye umri kati ya miaka 15 – 24 ni asilimia 0.2%.

(a) Je, serikali haioni kwamba ipo haja sasa ya kukamilisha uanzishwaji wa Baraza la Vijana haraka iwezekanavyo ili kunusuru hali ya vijana juu ya masuala ya ukimwi lakini pia janga la dawa za kulevya ikitilia maanani kwamba vijana ni nguvu muhimu katika siasa, uchumi na jamii.

(b) Serikali kupitia wizara husika inaahidi ni lini hasa Baraza la Vijana litakamilika na kuzinduliwa ili liwe chombo cha sauti ya pamoja ya vijana ambapo vijana watawasilisha malalamiko yao na serikali kuyapatia utatuzi wa haraka.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 82 lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, ni kweli Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dr. Ali Mohammed Shein katika hotuba yake ya uzinduzi wa Baraza la Nne la Wawakilishi aliahidi kukamilisha uanzishaji wa Baraza la Taifa la Vijana. Wizara yangu inawajibu wa kutekeleza ahadi hio.

(a) Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba ipo haja sasa kukamilisha uanzishwaji wa Baraza hilo la vijana haraka

iwezekanavyo. Wizara inaendelea na hatua za kukamilisha uanzishwaji wa Baraza hilo, baada ya mtaalamu muelekezi kuwasilisha rasimu ya Katiba ya Baraza hilo Wizarani, Kamati ya wataalamu imeundwa kuipitia rasimu hiyo, wataalamu wameipitia na kuna mapendekezo yao, baada ya kuyaingiza mapendekezo ya wataalamu wizara imerejesha rasimu hiyo kwa wawakilishi wa vijana, ambao nao wameongeza mapendekezo yao. Baada ya hatua hiyo wizara imewasilisha rasimu hiyo kwenye Kamati ya Uongozi ya Wizara.

Hivi sasa Waraka wa Rasimu hiyo umeshafikishwa katika kikao cha Makatibu Wakuu, baada ya maoni ya Makatibu Wakuu, Waraka wa Rasimu hiyo utawasilishwa Baraza la Mapinduzi. Nia ya wizara yangu ni kuunda Baraza la Vijana lenye uhakika litakaloweza kuwashirikisha vizuri vijana wa nchi yetu kwa maslahi ya vijana wenyewe na taifa kwa jumla na kuepuka, pamoja na kuupiga vita UKIMWI na kuendeleza mapambano dhidi ya madawa ya kulevya Zanzibar.

(b) Mhe. Spika, lengo la wizara ni kukamilisha uundwaji wa Baraza la Vijana la Zanzibar katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 *inshaallah* Mungu akipenda.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri huoni kwamba ipo haja ya kuwashirikisha wawakilishi ambao wanaingia katika Baraza hili kwa niaba ya vijana ili nao wakashiriki katika uundwaji wa Baraza hilo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa bahati nzuri wawakilishi wa vijana waliomo katika Baraza hili watapata nafasi nzuri ya kulijadili hili Baraza la Vijana wakati litakapoletwa hapa.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Waziri alipokuwa anajibu swali mama alisema kwamba tayari rasimu imeshapitiwa na wizara na pia wamewapelekea vijana waipitie. Je, hao vijana ambao wamepelekewa kuipitia ni vijana wa nchi nzima au ni kundi la vijana na kama kundi tu la vijana, vijana hao wamepatikana kivipi.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, hatuwezi kuchukua vijana wa nchi nzima tukawashirikisha katika kuandaa Baraza hili la Vijana, lakini kuna uwakilishi ambao ndio wanaohusika na ndio tuliowarejeshea ili watoe mapendekezo yao kwa niaba ya vijana wa nchi nzima.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, sasa hivi tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo kuwa inaongoza nchi yetu na Mhe. Waziri katueleza kwamba kuna pendekezo la kuunda Baraza la Vijana la Zanzibar. Kwa kuwa vyama vyote vya siasa vilivyopo kwenye nchi yetu kila chama kina Baraza lake la Vijana, hivyo kwa sababu Baraza hili linalotaka kuundwa ni Baraza la Vijana la Wazanzibari wote.

Je, kwa kuwa tuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa wizara yake imelizingatia suala hilo la umoja wa kitaifa. Na kama haikuzingatia Baraza hilo litaundwaje na sisi tunaka kujua hilo.

Mhe. Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwanza naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba sisi tunaunda Baraza la Vijana tumewashirikisha vijana sio kwa kupitia kwamba huyu ni nani na huyu ni nani. Lakini tumesema hili ni Baraza la nchi nzima kwa hivyo vyama mbali mbali vitaingia ikiwa ni NCCR, ikiwa CCM, ikiwa CUF wote wamo katika Baraza hilo.

Nam. 110

Bodi ya Mikopo

Mhe. Mohammed Said Mohammed – Aliuliza:-

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa nia njema imeanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ili kuwapatia fedha wanafunzi wa vyuo mbali mbali.

a) Je, serikali inadai kiasi gani fedha tangu kuanza kwa program hiyo hadi sasa.

b) Je, wahitimu wangapi wamerejesha fedha hizo tangu kuajiriwa.

c) Je, serikali ina mkakati gani wa kukusanya madeni ya wahitimu walioko kwenye ajira rasmi na zisizo rasmi, ambao waliosoma kwa fedha za Bodi ya Mikopo Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 110 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar imeanzishwa na sheria Nam. 2 ya 2011 kwa madhumuni ya kuwapatia mikopo ya fedha vijana wa Zanzibar wenye sifa za kujiunga na Vyuo cha Elimu ya Juu. Kabla ya hapo sheria ya Mfuko wa Elimu ya Juu ya Nam. 6 ya 2011 ilikuwa inatumika kwa ajili ya kuwapatia wanafunzi mikopo mbali mbali ya kusoma katika taasisi za elimu ya juu. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba kujibu kama ifuatavyo:-

a) Jumla ya bilioni 8.1 zimetolewa na serikali kwa ajili ya kuwakopesha wanafunzi 1910 kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2011 Disemba.

b) Hadi sasa hakuna hata muhitimu mmoja ambaye amerejesha fedha hizo toka zilipotolewa.

c) Hivi sasa wizara inatayarisha taratibu za kanuni za sheria iliyoanzisha Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu ya mwaka 2011, miongoni mwa kifungu cha kanuni hizo ni kifungu kinachofafanua utaratibu na ukusanyaji wa madeni ya elimu ya juu. Kanuni hizo zinatarajiwa kukamilika na kutumika mwanzoni mwa mwezi wa Februari, 2012. Vile vile Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu inaendelea kuorodhesha sehemu za kazi za wahitimu waliopata mikopo kwa nia ya kuwasiliana na waajiri wao mara tu kanuni za malipo ya madeni zitakapoanza kutekelezwa.

Lengo la Bodi ya Mikopo ni kufuatilia wanafunzi hao sehemu zote walipo katika sekta rasmi au isiyo rasmi na kuwataka warejeshe mikopo hiyo. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mohammed Said Mohammed: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa amekiri Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake ya msingi kuwa wizara inaandaa kanuni

madhubuti za kuweza kukusanya pesa hizo na pesa nyingi zimetolewa na serikali hivyo tunaishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Je, haoni iko haja sasa ya kufanya mpango huu wa haraka au kanuni zikawekwa haraka ili kukusanya fedha hizo ambazo wanafunzi wengi hivi sasa wamekosa fursa ya kupata mikopo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kanuni za Bodi ya Elimu ya Juu ziko tayari na tayari tumeshaziwasilisha kwa Mwanasheria Mkuu na tunatarajia itakapofika mwezi wa Februari kanuni hizo Mhe. Waziri atazitia saini na baada ya kutiwa saini kanuni hizo basi ufuatiliaji wa kukata madeni hayo utaanza mara moja kwa wale wakopaji ambao tushawatambua. Mhe. Spika, tuna wakopaji ambao tumewatambua kama 234, lakini kuna na wengine 1000 ambao majina na picha zao tayari tumezipeleka katika Ofisi za Vitambulisho ili kutambuliwa. Nakushukuru sana Mhe. Spika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Kwamtipura naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuanzia mwaka 2006 tayari imeshatoa mkopo wa Elimu ya Juu kwa wanafunzi karibu shilingi bilioni 8, lakini mpaka sasa hivi bado fedha wametuthibitishia kwamba hazianza kulipwa.

Mhe. Spika, kwa kuwa amesema wizara tayari wameshaanza kufanya huo utafiti wa kujua wanafunzi ambao waliokopeshwa fedha hizo, wamesema tayari karibu wanafunzi 200 tayari wameshapata majina yao, lakini kuna wengine zaidi ya 1000 wameshapata picha zao wamepeleka Idara ya Vitambulisho kwa ajili ya kutambuliwa.

Je, kwa kuwa tayari kanuni wameshatayarisha ambazo zitakazoweza kuwasaidia kuweza kukusanya hizo fedha na hayo majina ambayo tayari wameshayapata wanategemea kwamba kwa kila mwaka wizara itaweza kukusanya kiasi gani cha fedha ili kuwa na muelekeo wa kuweza kuwapa mikopo na vijana wengine ambao wanahitaji kwa hivi sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, mikopo hii inapitana kuna wanafunzi ambao wamesoma nje ya nchi hawa kawaida mikopo yao huwa ni karibu 70 milioni mpaka milioni 100, na kuna wanafunzi ambao wanasoma ndani ya nchi. Kwa hivyo, ukataji wa mikopo hii utalingana na ile pesa ambayo amechukua mkopaji na kwa hivi sasa siwezi kumwambia ni nani atakatwa kiasi gani kwa sababu viwango vya ukopaji ni tofauti.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kutokana na majibu ya Mhe. Naibu Waziri inaonekana kuna matatizo mara nyengine katika kuwatambua hawa ambao wanakopeshwa. Juzi tu Mhe. Spika, tumesoma katika magazeti upande wa Tanzania Bara Ofisa Mkuu wa chombo hiki cha umoja wa mikopo mmoja alifikishwa Mahakamani kwa kudanganya akiwa amejipatia karibu milioni 90 kutokana na kuingiza majina hewa aliowapatia mikopo.

Je, Mhe. Naibu Waziri hahisi kwamba inawezekana kuna tatizo kama hili katika bodi yake na pengine kuna haja ya kufanya uhakiki wa jumla ili kuona matatizo kama haya ambayo yameonekana upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano yasije yakatokezea hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli tuna matatizo ya kuwatambua hawa ambao tumewapa mikopo na matatizo yetu sifikirii sana kama yanalingana na yale ya Tanzania Bara, matatizo ambayo tunayo na tumeyabaini ni ile sheria ya mikopo ambayo tulikuwa tukiitumia ya Nam. 6 ya mwaka 2001 kanuni zake zilikuwa hazikuweka utaratibu mzuri wa kuwatambua wakopaji. Kwa mfano, Mhe. Spika, ilikuwa ni jina tu ambalo tulitaka kulijua kutoka kwa mkopaji na picha, ndio hii imetupa hali ngumu ya kuwatambua wenzetu hawa ambao wamekopa.

Mhe. Spika, lakini kwa sheria hii mpya ya 2011 sheria Nam. 2 tumeweka utaratibu mzuri kwa mfano kwenye kile kifungu cha 20 tunamtaka mkopaji lazima awe na kitambulisho cha Mzanzibari na ndio maana nilieleza hapa katika jibu langu mama kama hivi sasa tunashirikiana na wenzetu wa vitambulisho ili kwa kutumia zile picha na majina tuweze kuwatambua hawa wenzetu ambao wamekopa. Mhe. Nakushukuru sana.

Nam. 49

Ujenzi wa Mtaro wa Maji Taka

Mhe. Hamza Hassan Juma – Aliuliza:-

Namuuliza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa muda mrefu wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, wamekuwa wakisumbuliwa sana na maji hasa zinaponyesha mvua kubwa kwani mtaro unaotokea Darajabovu kupitia Mboriborini, Shaurimoyo hadi Saateni hujaa maji na kusababisha mafuriko makubwa sana na maji kuingia majumbani. Ni ahadi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kujenga mtaro huo kwa muda mrefu lakini hadi sasa hakuna dalili zozote za ujenzi wa mtaro huo.

(a) Je, Mhe. Waziri, ahadi ya Serikali imefikia wapi.

(b) Kama ipo Je, mradi huo unategemewa kuanza lini.

(c) Je, unawaeleza nini wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kuhusu mtaro huo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 49 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Spika, ni kweli wananchi wa Jimbo la Kwamtipura wamekuwa wakisumbuliwa sana na kutuama kwa maji ya mvua wakati wa mvua zinaponyesha, na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalijua vyema tatizo hili. Aidha, ahadi ya serikali bado ipo pale pale na naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba tujitayarishe kushirikiana na wananchi katika ujenzi wa mtaro huu kwa kupitia mpango wa kuimarisha huduma za miji Zanzibar (*Zanzibar Urban Services Program – ZUSP*). Msingi huu ambao ni mkubwa wenye urefu wa mita zipatazo 2789 utakaoanzia Darajabovu kupitia Shaurimoyo hadi Saateni. Mhe. Spika, msingi huo utakapokamilika kwa kiasi kikubwa utawaondoshea kero za kutuama kwa maji wakati wa mvua katika maeneo yatakayopita na maeneo ya karibu.

b) Kwa mujibu wa mpango kazi wa *ZUSP* kazi za ujenzi wa msingi huo unatarajiwa kuanza mwaka huu. Hata hivyo, hatua za awali za utekelezaji wa mradi zimeshaanza kama nilivyosema jana kwa mchakato wa ununuzi wa zana nzito na nyepesi ambazo zinatarajiwa kutumika katika uchimbaji na ujenzi wa mtaro wenyewe.

c) Mhe. Spika, serikali namuomba sana Mhe. Mwakilishi na wananchi wa Kwamtipura kwa ujumla kuwa na subra wakati taratibu zinaendelea za kupatikana mkandarasi wa ujenzi, vile vile tunaomba wananchi wa jimbo hilo kushirikiana na Manispaa katika kuhifadhi, kulinda na kuhakikisha kwamba mtaro utakaojengwa unabaki katika hali ya safi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nataka nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kutilia maanani dhiki ya wananchi wa

Jimbo la Kwamtipura na vile vile serikali na hasa kwa kuwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alitilia nguvu hasa wakati wa kampeni aliwaahidi wananchi wa Jimbo la Kwamtipura kwamba angeliweza kukamilisha kiu ya wananchi wa jimbo hilo kwa kujenga mtaro huu wa Darajabovu, Shaurimoyo hadi Saateni.

a) Mhe. Spika, Mhe. Waziri amesema kwamba mradi huu unategemea kuanza mwaka huu na tunavyofahamu ni kwamba mtaro ni sehemu ambayo inapita maji kwa kweli mtaro ule unapita maji mengi sana hasa wakati wa mvua. Je, kwa kuwa mpaka sasa hivi bado hatujaona harakati zozote za ujenzi na wala mkandarasi bado mpaka sasa hivi hajatafutwa, hatuoni huo ujenzi utakapoanza utakuja ingiliwa na msimu wa mvua ambapo inaweza ikapelekea kwamba mtaro huo ukakamilika kwa wakati uliotarajiwa au ukaja ukachelewa na pengine hizo gharama ambazo zinazotarajiwa kutumika zikaja zikawa zisitoshe.

b) Mhe. Spika, tumesikia kwamba fedha hizi ambazo tayari kwa mashirikiano na World Bank kwamba tayari fedha hizo zimeshatengwa kwa ajili ya mtaro huu. Lakini vile vile tumesikia kwenye vyombo vya habari kwamba kuna maagizo mengine au kuna maelekezo mengine ya serikali kwamba fedha hizo zitumike na maeneo mengine ambapo pengine fedha hizo zililengwa zaidi katika miradi. Je, fedha hizo za World Bank kama zitatawanywa katika maeneo mengine tunahakikisha kwamba fedha hizi zilizotarajiwa kutumika zitakuja kuweza kutosha. Na kama hazikuweza kutosha mtaro ukija ukijengwa nusu je sehemu iliyobakia haitokuwa hasara kwa serikali na wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwanza kwa niaba ya serikali nakubali kuzipokea pongezi uliotupa za matayarisho au za uamuzi wa kujenga msingi ule. Ni kweli kwamba hata hivi sasa wakati haujajengwa lakini ukitizama wakati wa mvua msingi ule unavyojaa maji na unavyofurika kwa kweli iko haja kwamba lazima ufanyiwe kazi tena ili kusitiri hali ya maeneo yale. Lakini kuchelewa kwa msingi au kuchelewa kwa kuanza kazi hasa kwa kweli kumetokana na matatizo ya kiufundi yaliyotokezea wakati wa kupata hao wakandarasi na wanunuzi wa vitu, nafikiri sote tumefahamu taratibu za *World Bank* lakini ngumu kidogo, ni ngumu na kulikuwa na vikwazo kidogo vya wenzetu katika Wizara ya Fedha kule kupata saini fulani, zilituhangaisha na mpaka kupata saini ya Mwanasheria Mkuu tulichukua zaidi ya miezi sita ambazo lazima tulikuwa tuzipate *procurement process* iendelee.

Kwa hivyo, nasema ni vikwazo vya kitaalamu lakini tushakwamuka sasa mchakato mzima ule wa manunuzi na kupata wakandarasi tenda zimeshafunguliwa na mambo yanaendelea. Tutachelewa kidogo lakini tusiwe na wasi wasi Mhe. Hamza Hassan na wananchi wa Kwamtipura hilo litafanyika.

Naomba jibu la mwisho nimhakikishie kwamba, hakuna fedha yoyote katika mradi huu iliyokisiwa kwa kazi za mradi huu zitapelekwa kwengine. naamini mtakumbuka kwenye *budget speech* yangu nimetaja pesa zile dola za Kimarekani 38 milioni na kazi zake ni nyingi kabisa na mitaro ni mingi. Kwa hivyo, sijui na hii *inflexion* iliyopo kama zitakuja kututosha, hivyo hakuna wasi wasi wowote wa pesa hii kutumika kwengine. Lakini kama zitapunguka basi serikali yet ipo tutafanya mpango tutashirikiana na *World Bank* lakini kazi hii ikamilike. Naomba ni mhakikishie Mhe. Mwakilishi asiwe na wasi wasi.

Mhe. Ali Salim Haji: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Tutakumbuka kwamba katika kipindi kifupi kilichopita ndugu zetu wa Manispaa waliweza kutengeneza mitaro kupitia Benki ya Ujerumani katika *Phase II*, mitaro hiyo kuna mtaro kutoka Amani/Ziwatuwe na Kwahani/Kilimani. Lakini kinachoonekana kwamba mitaro ile haikuwa na ubora hata kidogo na imepelekea kuwa ufanisi wa kazi hiyo haukuwa mzuri.

Je, Mhe. Waziri atatuhakikishia vipi katika hii awamu mpya itakayokuja wamejipanga vipi ili lile ambalo limetokea katika mradi huu mara hii lisitokee.

Mhe. Spika: Hivi mradi huu ni mmoja pamoja na ule wa Kwamtipura?

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Ni mradi mmoja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kwa kawaida mradi wa ujenzi wowote kunakuwa na msimamizi ambaye anafuatilia kila hatua ya mjenzi na hata ile pesa yake yule mjenzi haipati kama hakuna hati ya kuthibitisha ubora na ukamilifu wa ujenzi ule. Kwa hivyo, naomba nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kama ilitokea wakati huo basi ilikuwa bahati mbaya, lakini safari hii tutakuwa wasimamizi wa karibu zaidi. Kwa sababu huo mradi ni wetu, ni wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hizi pesa ni za mkopo tumekopa sisi. Kwa hivyo, tutahakikisha kwamba kweli lina ubora.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. Pamoja na nia nzuri ya serikali

na Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri aliyojibu ni nia nzuri tu ya kujenga mtaro huo. Lakini Mhe. Spika, kuna vidaraja ambavyo vimevunjia zaidi ya miaka mitano au sita na vidaraja hivyo vimeziba njia za maji ambayo vinasababisha maji kujaa wakati mwengine kuingia katika majumba ya watu.

Sasa namuomba Mhe. Waziri, kwa sababu mradi huo bado kujenga lakini zile daraja ni dharura na ni njia ambayo inapita watu na imeziba taka zote zinajaa pale, namuuliza Mhe. Waziri atachukua hatua ipi ya msingi ya kuvijenga vidaraja vile ili kuwanusuru wananchi wapate njia yao na maji yasiingie kwenye nyumba.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubali kwamba ni kweli kuna vidaraja vile ambavyo vinatumika watu kupitisha watu. Kwa bahati mbaya vingi vimekuwa vibovu na kama anavyosema kabla ya ujenzi kamili wa mitaro haujakamilika iko haja ya kuvitengeneza. Nakubaliana na yeye suala hilo na nafikiri tutalishughulikia tutalifanya kuhakikisha kwamba angalau vinaweza kupitika kabla ya ujenzi kukamilika. Nakubali ushauri wake.

Nam. 81
Matibabu ya Saratani Zanzibar

Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Aliuliza:

Katika Mkutano wa Tano, Kikao cha Kwanza cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kilichofanyika tarehe 8/11/2011 Dodoma, Mhe. Naibu Waziri wa Afya wa Tanzania wakati wa kipindi cha maswali na majibu alisema kwamba alifanya mazungumzo na Mhe. Waziri wa Afya wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Mhe. Juma Duni Haji na alimueleza kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ina mpango wa kuanzisha huduma za kutoa matibabu ya Saratani Zanzibar badala ya wagonjwa wa Saratani Zanzibar kufuata huduma hizo Tanzania Bara.

(a) Je, Mhe. Waziri wa Afya anakubaliana na maelezo hayo yaliyotolewa Bungeni na Mhe. Naibu Waziri wa Afya wa Tanzania.

(b) Je, Mpango huo wa kutoa matibabu ya Saratani hapa Zanzibar unategemea kuanza lini.

(c) Je, serikali ina mikakati gani ya kutoa elimu kwa kinamama wa Mijini na Vijijini juu ya uelewa wa maradhi ya Saratani sambamba na kuwashajiisha kinamama hao kufanya uchunguzi wa mara kwa mara (*check up*) wa Saratani ya matiti na Saratani ya kizazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 81 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo;-

(a) Mhe. Spika, ndio Mhe. Waziri wa Afya anakubaliana na maelezo hayo yaliyotolewa Bungeni na Mhe. Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Tanzania.

(b) Mpango wa kutoa matibabu ya Saratani hapa Zanzibar kwa lile linalowezekana linafanyika siku zote kwa baadhi ya maradhi mara tu mgonjwa anapobainika na tatizo hilo.

(c) Serikali ina mikakati ya kutoa elimu ya afya sio kwa akinamama tu au saratani peke yake, bali inafanya kazi ya utoaji wa elimu ya afya kwa maradhi yote mijini na vijijini.

Ili hayo yaweze kutekelezwa kuna sheria ambazo zinahitaji kufanyiwa marekebisho na nyengine kuundwa.

i. Wizara inafanya mapitio ya sheria ya afya ya jamii na kutayarisha rasimu ya sheria ya baraza la kuwasajili mabwana na mabibi afya (zipo katika ngazi ya makatibu wakuu) na kufanya utafiti kuhusu maradhi yasiyokuwa ya kuambukiza ikiwemo saratani.

ii. Kwa upande wa Kitengo cha Elimu ya Afya kuna mkakati wa kukiimarisha kitengo chenyewe na kwa kuwashirikisha washirika wa maendeleo kwa ajili ya kugharamia gharama za utoaji wa elimu hiyo kupitia njia mbali mbali na ununuzi wa vifaa vya kufanyia kazi hiyo. Pia, kazi inayofanyika sasa ni kutayarisha na kurusha matangazo kupitia radio na televisheni, elimu ya afya maskulini, kupitia kampeni mbalimbali za kitaifa kwa kutumia taasisi zisizokuwa za kiserikali na za kidini.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa amekiri kwamba wanatoa matibabu haya ya saratani nilikuwa nina *interest* ya kujua kitengo hiki kiko wapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa kawaida kitengo kinatakiwa kiwepo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kama hospitali ya rufaa. Hivi sasa

tuko katika maandalizi ya kuandaa kitengo hicho, lakini matibabu yanafanyika katika Hoapitali ya Mnazi Mmoja katika idara mbali mbali inategemea na saratani ya aina gani. Kuna kitengo cha mama na mtoto, kule ambapo huwa wanachunguzwa kensa ya shingo ya kizazi au matiti, sehemu ya upasuaji wanachunguza na maabara. Kwa hivyo, idara hizo tatu huwa zinashirikiana kutegemea na aina gani ya kensa inayotakiwa kuchunguzwa.

Pia katika Idara ya Upasuaji hiyo ndio inayoshughulika na matibabu kama ni operesheni inafanyika na huwa inatoa matibabu kama ni ya vidonge au ya kupitia kwa njia ya mishipa ya damu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba niulize swali dogo tu la nyongeza. Kwa kuwa tuna uzoefu kwamba wagonjwa wengi wa saratani wanaofika Hospitali ya Mnazi Mmoja hupelekwa Muhimbili na hatimaye hapo Muhimbili wakaambiwa waende *Ocean Road*. Je, isingekuwa vyema kwa waziri akatangaza tu kwamba hakuna kitengo wala matibabu hayo hayatolewi hapo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Kwa kuwa wanawake mbali na kwamba ni muhimu sana katika uchumi wa Zanzibar, na kwa kuwa hivi sasa kensa ya kizazi pamoja na matiti imekuwa ni tatizo kubwa kwa kinamama. Je, ni lini serikali itaandaa mpango wa kitaifa kama ule wa kupambana na malaria, UKIMWI, wakaandaa programu maalum ya kupima hawa kina mama saratani za kizazi kama vile inavyofanywa kwa mambo ya UKIMWI na Pepopunda.

Mhe. Naibu Waziri wa AFya: Mhe. Spika, ni kweli baadhi ya wagonjwa wanapogunduliwa na maradhi hayo huwa wanapelekwa Muhimbili au *Ocean Road*. Hiyo inategemea na kipi kinachotakiwa kufanyika, nimesema kwamba kuna baadhi ya mambo ambayo yanaweza kufanyika katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini mengine hayafanyiki kwa sababu ya ukosefu wa vifaa vinavyohitajika kufanyiwa hivyo. Muhimbili na *Ocean Road* wana vifaa hivyo kwa hivyo inabidi wagonjwa wapelekwe Muhimbili au *Ocean Road* kwa ajili ya kufuatilia matibabu yale ambayo hapa kwetu hayawezekani.

Lakini tutakapokuwa na kitengo hicho cha kensa matibabu yote hayo yataweza kufanyika hapa hapa na wakati Hospitali ya Rufaa itakapokuwa na kitengo hicho ambacho kinaandaliwa hakutokuwa tena na haja ya watu kuwapeleka Dar es Salaam kwa ajili ya matibabu hayo. Hilo la kwanza.

La pili kuhusu masuala ya kuwachunguza kinamama. Suala la kuwachunguza kinamama linafanyika kwa Bara wenzetu wana kitengo kisichokuwa cha serikali *NEWATA* wanachunguza kwa utaratibu huo wanaungwa mkono na wafanyabiashara pamoja na serikali. Hapa kwetu ili hayo uweze kuyafanya

inatakiwa aidha iwepo *NGO* inayohusiana na hilo ili sisi tuweze kuwasaidia. Au tusibiri mpaka mpango kamili utakapokamilika wa kuhudumia wagonjwa wa kensa ndipo tutakapoweza kufanya hivyo. Lakini hata hivyo, hayo yameshawahi kutendeka.

Mwaka jana tu watu walipimwa kwa kushirikiana na maabara yetu pamoja na Hospitali ya Aghakan walikuja wakawapima akinamama matiti, watu 950 walipimwa na kati ya hayo 10 walikutwa na matatizo, wanne walikutwa tayari wana kensa ambayo imefikia mbali na wanne walikuwa wana wasi wasi kwa hiyo wakaanza kupimwa ili kuhakikisha kwamba tatizo hilo wanalo ama laa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, kunipa nafasi kuuliza swali moja la nyongeza. Namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa wengi wetu humu na sisi tumo wanawake. Je, ni dalili gani za magonjwa haya ya kensa ya titi la mama. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, matatizo makubwa yanayosumbuwa wanawake kama kensa. Kuna kensa ya shingo ya kizazi na kensa ya matiti, ingawa matiti hata wanaume wanaweza wakapata. Sasa tuanze na kensa ya kizazi.

Kensa ya Kizazi. Kensa ya kizazi mara nyingi huwa inajitokeza mtu kupata maumivu chini ya kitomvu baadae huwa mara nyingi anatokwa na damu isiyosimama, sio siku zake za hedhi wala siku za kawaida ni mfululizo, anapofanya kitendo cha kujamiiana huwa anatokwa na damu. Kwa hivyo, hicho ni kiashirio cha kusema kwamba huyo mtu anaweza kuwa ana kensa ya kizazi.

Kensa ya matiti huwa kunatokea vivimbe katika titi au kama imechelewa kunatokea kidonda katika titi au katika sehemu ile ya ncha ambako kuna kile kinyonyeo cha lile titi huwa linajikunja linakuwa kama gamba la limau. Pia kunaweza kuwa kukatoka damu kwenye chuchu. Kwa hivyo, hizo ni dalili za kensa za titi.

Nam. 86

Matengenezo ya Nyumba Mji Mkongwe

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Maeneo ya Mji Mkongwe ni sehemu ya makaazi ya watu. Hii ina maana kuwa mahitaji ya watu yapo kama kawaida katika kila nyanja ikiwemo nyumba na makaazi kwa ujumla. Yaani, watu watahitaji kujenga nyumba katika maeneo haya na pia kuzifanyia matengenezo zile ziliopo.

(a) Je, Mhe. Waziri, kuna taratibu zipi za kufuatwa na mtu ambae anataka kujenga au kuifanyia matengenezo makubwa nyumba yake katika Mji Mkongwe.

(b) Ni lini serikali itaziweka wazi taratibu hizi ili zieleweke na hasa kwa watu wanaotaka kujenga au kutengeneza nyumba zao katika sehemu zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati - Alijibu:

Mhe. Spika kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam**.** 86 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mtu yoyote anapotaka kujenga ama kuifanyia matengenezo makubwa nyumba yake anapaswa kuomba idhini kwa Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe kimaandishi na kuelezea dhamira yake, pamoja na kuambatanisha vielelezo vya umiliki ama ukodishwaji. Mamlaka baada ya kufanya ukaguzi wa eneo husika pamoja na kulijadili ombi hilo, humjibu muombaji kuwa ombi lake limekubaliwa au limekataliwa pamoja na sababu za kukataliwa kwake. Kama limekubaliwa hupewa ushauri kuhusiana na matengenezo hayo.

(b) Mhe. Spika, taratibu hizi ziko kwa watu wote wanaotaka kujenga au kutengeneza nyumba zao katika eneo la Mji Mkongwe, lakini nayo Mamlaka kwa upande wake inajitahidi kuelimisha wananchi kupitia semina mbalimbali pamoja na kuwatumia masheha katika suala hili.

Mhe. Jaku Hashim Ayouba: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Ni vigezo gani vinavyotumika katika eneo la Mji Mkongwe wengine kuuziwa zaidi ya ghorofa tatu na wengine kutoruhusiwa wakati sheria ya uhifadhi w ana Mji Mkongwe ni moja tu.

Pili, kwa Katiba ya Zanzíbar ya mwaka 1984 inaeleza kwamba wananchi wote wana haki sawa mbele ya sheria. Je, watendaji wanazingatia vipi matakwa ya sheria ili kuepusha malalamiko kwa wananchi.

Tatu, serikali ina msimamo gani juu ya majengo ya chini kuvunjwa na kupandishwa ghorofa sio kwenda kinyume na Mji Mkongwe huku. *(Kicheko)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza swali ni kwa nini wengine wanaruhusiwa kujenga ghorofa ya tatu na wengine wanazuiliwa? Ujenzi katika Mji Mkongwe unategemea kwanza maombi, ramani iliyoletwa na hatimaye kibali kilichotolewa. Kama ombi la ghorofa moja ni la ghorofa moja, mbili maana yake mbili na tatu maana yake tatu.

Wengine wanaopewa ruhusa ya kujenga ghorofa tatu au zile nyumba zilioko ambazo ni za ghorofa tatu, zile zilijengwa kabla ya kupitishwa sheria Nam. 4 ya mwaka 2010 ya Mji Mkongwe. Kwa hivyo, baada ya kupitishwa sheria hiyo ambayo imetoa maelezo yote kwa kikamilifu aina ya nyumba zinazostahiki kujengwa Mji Mkongwe basi sheria hiyo inafanya kazi na hii sheria haina ubaguzi.

Swali lake la pili namuomba alirejee sikulifahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, nimeuliza kwa kuwa Katiba ya Zanzíbar ya mwaka 1984 inaeleza wananchi wote wana haki sawa mbele ya sheria. Je, watendaji wanazingatia vipi matakwa ya sheria ili kuepusha malalamiko kwa wananchi.

Tatu, serikali ina msimamo gani wa majumbe ya chini yanayovunjwa na kupandishwa ghorofa. Je, huku si kwenda kinyume na Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, katiba ni sheria mama lakini badea kuna sheria zinazotungwa na Baraza hili, hizo mimi sitaki niziite sheria baba au nini lakini sheria. Sheria iliyotungwa mwaka 2010, Sheria Nam. 4 imetiwa saini baada ya kujadiliwa na Baraza la Wawakilishi ilitiwa saini tarehe 26 Julai, 2010 na hapo sasa kuwa ni sheria kamili baada ya kupata *assentment* ya Rais.

Sasa kama sheria hii tuliiipitisha na ikapata *assentment* ya Rais, sheria hii haikiuki matakwa ya katiba vyenginevyo ingekatalika. Hakuna sheria inayosimama mbele ya katiba, katiba ndio huwa sheria kuu. Sheria hii imesimama baada ya kutiwa saini na ndio inayofuatwa na baadae tukatunga kanuni zinazotoa maelekezo sasa ya utekelezaji wa sheria hii. Kwa sababu hiyo, hapa hapana suala kwamba sheria hii inakiuka Katiba ya Zanzíbar. Suala la tatu la nyumba za chini na za juu kidogo alirejee nipate kuelewa vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, kwa mara ya tatu na ya nne narudia tena swali hili. Mhe. Waziri kuna nyumba za chini zimevunjwa na vimejengwa ghorofa zaidi ya tatu. Je, kuzivunja nyumba zile si kwenda kinyume na Mji Mkongwe.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nyumba ya chini inapovunjwa kwa kujengwa nyumba ya juu inategemea maelekezo ya sheria na kanuni. Kama kuna nyumba ya aina hiyo ya chini ilivunjwa pengine imevunjwa kwa sababu ya kuhatarisha maisha ya wananchi majirani pamoja na hao wanaokaa katika nyumba hiyo. Kwa kufanya hivyo si kukiuka sheria lakini kulinda usalama wa wananchi.

Lakini pamoja na suala hilo, mimi sikufahamu kwamba kuna nyumba ya chini ilivunjwa bila ya kufuata kanuni na sheria na kujengwa nyumba ya juu. Namuomba Mhe. Mwakilishi mimi na yeye tufuatane baada ya kikao hiki tukaikague hiyo nyumba iliyojengwa kinyume na utaratibu.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri swali la nyongeza. (a) Mhe. Spika, suala lililoulizwa mimi naomba nirejee kwamba, hatuzungumzii sheria Nam. 4 ya mwaka 2010 kwamba inakiuka Katiba, lakini tunachohoji kwamba Katiba imeweka kifungu kinachokataza ubaguzi katika utekelezaji wa sheria ya utendaji wa serikali kwa jumla. Kinachoonekana katika Mji Mkongwe ni kwamba, naomba niseme taratibu ili Mhe. Waziri anielewe, kinachoonekana katika Mji Mkongwe ni kwamba kuna ubaguzi katika utekelezaji wa sheria hii. Kwa sababu kunakuwa na watu wenye uwezo ambao hao mara nyingi wanaruhusiwa kukiuka sheria.

Kwa mfano, liko jengo lililokuwa karibú na Skuli ya Shangani au Idara ya Mitaala inajengwa hoteli ambayo ina ghorofa nne hivi sasa, lakini wananchi masikini wa kawaida wanapotaka kufanya marekebisho madogo tu mara nyengine wanaingilia kati na Mamlaka ya Mji Mkongwe na kuvunjiwa hata kutakiwa kurejesha hali kama ilivyokuwa pale Mwanza. Sasa ndio tukauliza kwa nini inaonekana kuna ubaguzi katika utekelezaji wa sheria sio kwamba sheria imekiuka taratibu.

Pili naomba nimuulize Mhe. Waziri ana kauli gani kuhusu jengo ambalo liko katika eneo la Uwanja wa Malindi au Darajani pale ambalo lilijengwa na hivi sasa liko katika ghorofa ya tatu. Karibuni Mamlaka ya Mji Mkongwe ilivunja ghorofa ya tatu lakini baadae tukaona ghorofa hiyo inaendelea kujengwa. Tunataka kuhoji serikali kwamba, kuna upinzani gani na gani katika vyombo vya utendaji vya serikali kwamba siku moja inavunjwa na siku ya Pili inaendelea kujengwa tena. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, namuomba Mhe. Ismail Jussa anifahamu kwamba na mimi nimefahamu kama alivyofahamu yeye, kwamba sheria haina ubaguzi lakini vitendo vya kuitekeleza sheria ndio vyenye ubaguzi. Nataka niseme kwamba vitendo vya wizara yangu vya kutekeleza sheria Nam. 4 ya mwaka 2010 vitendo hivi havina ubaguzi, vitendo vinaambatana na sheria na kanuni zenyewe.

Suala la kwamba huko Mji Mkongwe kuna jumba moja linajengwa la ghorofa nne hili nalipokea tena kwa mikono miwili. Kwa sababu sheria yetu inakataza kufanya hivyo na tutalishughulikia, tena tutalishughulikia kwa kushirikiana na Mwakilishi wa Mji Mkongwe ambaye ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu.

Swali lake la pili, nataka nitoe ufafanuzi kama ifuatavyo: Kujengwa, kuzuwiwa kujengwa na kuzuwiwa kunatokana na ukaidi wa huyu aliyepewa Kigali kujenga hiyo nyumba. Kumbukumbu ninazo za kutosha hapa, Kigali cha mwanzo kilichotolewa kwa huyu anayejenga nyumba hii kilifuata ramani aliyoiwasilisha kwenye *authority* ya Mji Mkongwe. Ramani hii ilikuwa ya kujenga ghorofa moja. Ujenzi ulipoanza na kwa kweli ombi la awali lilikuwa ni kujenga *kiosk* cha kuuzia kama ni *ice-cream* au bidhaa nyengine pale chini.

Maombi yakenda yakarudi kwa Mkurugenzi wa Mji Mkongwe akaweka msimamo ombi ni kujenga *kiosk* chini na sio ghorofa moja, wala mbili, wala tatu. Hatimae Waziri aka-*over rule* akatoa agizo la kwamba apewe kibali cha kujenga nyumba ya ghorofa moja. Ikaletwa ramani, likaletwa ombi, ramani ndio hii hapa ya ujenzi wa ghorofa moja.

Hatimae kilipotoka kibali kukajengwa *balcony* kwenye ghorofa moja kinyume na ruhusa na kinyume na utaratibu. Ikatoka *stop order* ya kwanza hii, kuna *stop order* nne zimetolewa katika ujenzi wa nyumba hii. Ilipotoka *stop order* akatakiwa aondoshe nyumba, aondoshe mbao za kujenga *balcony* na kadhalika akafuata ule utaratibu. Lakini baadae akaongeza ghorofa moja sasa zikawa ghorofa mbili, narejea tena ombi ni la ghorofa moja. Ikatoka *stop order* bwana huyu akaendelea kujenga na akajenga kwa kwenda Baraza la Manispaa kuchukua *authority* ya kujenga. Kama kawaida ya Manispaa tunavyowajua wakatoa *authority* kinyume na sheria. Baraza la Manispaa hawahusiani na kutoa *authority* ya ujenzi Mji Mkongwe.

Utaratibu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, kifungu cha 58(3) kinasema "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu. Au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika." Mhe. Spika, kuhusu *kiosk* pana warka uliotolewa kisheria na kujenga nyumba. Kama kiosk huwezi kupewa *document* kama hiyo iliyokuwa halali aliyosema Mhe. Waziri. Naomba athibitishe.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kujua utaratibu. Nadhani ni vyema Mhe. Mjumbe ange-*declare* kama ana *interest* katika suala hili.

Mhe. Spika: Mimi nafikiri ninavyoona Mhe. Waziri pale majibu anayoyatoa anatoa na vielelezo alivyonavyo na anaelezea kwamba ombi la awali lakini hayo maombi inaelekea yalikuwa yanakwenda hatua kwa hatua. Hatua ya

kwanza ombi la awali anasema ilikuwa *kiosk* inawezekana hiyo hakuleta karatasi inayothibitisha hilo. Lakini ombi la pili kulikuwa na *overruling* ya Waziri nadhani wakati huo ameridhia kwamba ruhusa ilikuwa ni ya ghorofa moja kama nilifahamu sawa sawa. Halafu ikaendelea ghorofa ya pili kwa kupata *authority* ya Baraza la Manispaa ambayo kisheria haina uwezo huo ndivyo nilivyofahamu mimi.

Nadhani tumuachie Waziri aeleze vile anavyoelewa kwa mujibu wa taratibu zilivyo. Sasa kama kuna jambo jengine hapo baadae hili nadhani linaweza likaja swali jengine baadae la msingi kuhusiana na jambo hili. Nimruhusu Waziri aendelee.

Utaratibu

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, kifungu cha 58(4) kinasema "Ni marufuku kwa Mjumbe yeyote kusema jambo lolote ambalo linangojea uamuzi wa Mahakama. Mhe. Spika, kwa sababu jambo hili kuna taarifa kwamba liko Mahakamani nadhani kuendelea kulijadili hapa ni kukiuka ibara ya 58(4). Kwa hivyo, tunaomba Mhe. Waziri asitishe kujibu suala hili mpaka pale Mahakama itakapopitisha maamuzi.

Mhe. Spika: Hiyo sasa ni hoja nyengine ambayo kweli taratibu zetu za kanuni zinakataza kwamba jambo ambalo liko Mahakamani basi lisiendelee kujadiliwa hapa ika-*prejudice* hiyo maamuzi ya Mahakama.

Ukweli wa mambo suala hili limechupia kutokana na ile mapana ya Mji Mkongwe na hili jengine lililoingia kuhusu nyumba hiyo uwanja wa Malindi nayo iko katika eneo la Mji Mkongwe nafikiri ilikuja katika utaratibu huu.

Kimsingi sina hakika kama Waziri alikuwa anaelewa hivyo, lakini kama kuna taarifa suala hili liko Mahakamani mimi nadhani tuache kulijadili.

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, taratibu zinazoletwa hapa na ukaziruhusu ni taratibu zinazokwepa ukweli usielezwe. Swali hili maadam limekuja kwenye Baraza la Wawakilishi kwenye *order paper*, limeulizwa swali la msingi, umeniruhusu nitoe maelezo ya nyongeza.

Mhe. Spika, taratibu za kiujanja ujanja usiruhusu. Mimi baada ya kuliona swali hili katika *order paper* nilijua haliko Mahakamani na ndio maana limeletwa katika *order paper*. Sasa nani hakufuata utaratibu wa huo utaratibu unaozungumzwa kila wakati mimi simjui. Mimi najibu swali lililoulizwa na mhusika akauliza swali la nyongeza pia najibu. Mhe. Spika, niruhusu nijibu mpaka nimalize nazuia utaratibu.

Mhe. Spika: Unajua ni kweli kabisa inawezekana ikawa tunazungumza kitu ndani ya chombo hichi bila ya kuelewa kama kuna suala la Mahakamani na nadhani ndivyo ilivyokuwa hapo mwanzo. Swali la msingi halikuwa linahusiana na hasa nyumba hii ambayo yenyewe sasa kumbe kwa taarifa iliyotolewa ina kesi Mahakamani. Sasa kipande cha swali hili ambalo lina kesi Mahakamani ndio ambalo sasa inabidi tulizuie kungojea maamuzi ya Mahakama na hiyo ndio kanuni zetu zinavyotwambia hivyo. *(Makofi)*

Nadhani Mhe. Mwanasheria Mkuu anaweza akatusaidia kwa sababu inaweza ikaingilia maamuzi hatimae ya Mahakama kutokana na kile kitakachotoka hapa. Lakini mtazamo wa kanuni ulikuwa ni huo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nadhani kanuni zetu ziko wazi kwamba kama suala liko Mahakamani sio tu kwamba linaweza au haliwezi kuzungumzwa lakini kanuni zimesema wazi kwamba hairuhusu Mjumbe yeyote kuongelea suala ambalo liko Mahakamani. Kwa hivyo, ni kweli inaweza ikatokea likaletwa ama swali au ikaletwa hoja ambayo pengine Mjumbe aliyeleta hoja na anayejibu hana taarifa kwamba liko Mahakamani. Pengine na Baraza pia halina taarifa kwamba liko Mahakamani.

Lakini mtakapopata taarifa na Spika au anayeongoza kikao akaridhika kwamba liko Mahakamani, ni wajibu kufuata kanuni zetu kwamba hilo suala haliruhusiwi kuzungumzwa katika kikao hichi. Lakini suala linakuja pale pale pia kwamba kazi ya ulinzi wa kanuni hizi ni ya kwetu sote. Kwa hivyo, pengine aliyeuliza lile swali akijua liko Mahakamani na bado akauliza swali nadhani ni muhimu kusisitiza kwamba yeye mwenyewe hakupaswa kuuliza hilo swali kama alikuwa ana taarifa ya kwamba suala liko Mahakamani.

Mhe. Spika: Nimeiona *concern* ya Mhe. Waziri alipokuwa anajibu, hapa sio Mhe. Waziri kwamba amekosea hili, yeye alikuwa anajibu kwa mujibu wa swali alioulizwa. Kwa bahati mimi sikuwa na taarifa, lakini kuna Mjumbe yeye anayo taarifa kwamba jambo hili liko Mahakamani ametujulisha. Kwa mujibu wa kanuni zetu inabidi tu-*stop from there.*

Sasa ili kulinda hii kanuni ambayo inakataza kuzungumza jambo lolote ambalo liko Mahakamani. Mhe. Waziri kwa kuwa wewe hukuwa na taarifa hiyo hukukosea hivyo. Pengine mheshimiwa aliyeuliza swali hakuwa na taarifa hiyo hajakosea hivyo, hapa hatumtafuti mkosa lakini mwenye taarifa kwamba jambo hili liko Mahakamani sasa huyo anapaswa kulieleza Baraza hili ili tuwe tunakwenda kwa mujibu wa kanuni zetu. Baada ya taarifa hiyo ndio tukasema kwamba basi tusiendelee kujadili suala hili ili tufuate kanuni ambazo sote tunapaswa kuzilinda.

Kwa hiyo, nyongeza ya swali lililokuja haidhuru liko ndani ya Mji Mkongwe lakini halihusiani na lile swali mama hii tunaomba radhi kwamba lisiendelee. Baada ya hayo machache nadhani tuendelee. Kwa hili *ruling* sasa imeshatoka, Spika akitoa *ruling* kama hukuridhika nayo uende kwenye Kamati ya Maadili ushtaki huko.

Nam. 37

Haki ya Wananchi kupata Habari

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza**:**

Katika kutekeleza MKUZA Klasta ya Pili inaelezwa kuwa suala zima la kuimarisha utawala bora na moja kati ya utekelezaji wake ni uhuru wa Vyombo vya Habari na haki ya wananchi kupata habari.

(a) Kuna mapendekezo yeyote uliyoyapata ya wadau kuhusu Mswada wa Haki ya Kupata Habari katika Wizara yako.

(b) Kama umeyapata Wizara yako imeshayafanyia kazi na kuyatolea maamuzi.

(c) Maamuzi hayo ni yepi.

(d) Je, kama yamekwama Wizarani kwako unawaambia nini wanahabari pamoja na wadau wa habari.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:**

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 37 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa Wizara yangu imepokea mapendekezo ya Mswada wa Haki ya Kupata Habari iliyowasilishwa na *MCT*.

(b) Mhe. Spika, Wizara yangu imefanyia kazi kwani baada ya kupokea mapendekezo hayo, iliyachambua na kuyatafakari na hatimae kugundua zipo kasoro zinazohitajika kufanyiwa kazi.

(c) Mhe. Spika, maamuzi yaliyofikiwa na Wizara yangu ni kuandaa mikakati ya kuondosha kasoro zilizopo ikiwa ni pamoja na kuweka wigo mpana zaidi wa ushiriki wa wadau wengi zaidi wakiwemo wamiliki wa vyombo vya habari vya Unguja na Pemba.

(d) Mswada huu haujakwama Wizarani, isipokuwa nawashauri wadau wa habari wajiweke tayari kutoa maoni yao kwa ufasaha, uwazi na bila ya hofu wakati utakapofika wa kuandaa Mswada huu wa Sheria ya kuleta uhuru zaidi wa vyombo vya habari.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza kwa ruhusa yako naomba Mhe. Naibu Waziri anapojibu hili swali ile *mic* aisogeze ili yale maneno yaingie na *mic* iweze kupokea vizuri. Baada ya taarifa hiyo Mhe. Spika, naomba sasa nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Spika, mapendekezo ya wadau wa habarí kupeleka mswada kwa Waziri ambao walikuwa wanataka uletwe Barazani ili upitishwe uwe sheria kwa ajili ya kuwepo na Sheria ya Haki ya Kupata Habari.

Mhe. Spika, suala hili lipo kwa muda mrefu wizarani na kimsingi wananchi wanajitahidi pale serikali inapoona inachelewa hasa kutunga sheria ambayo itawapa haki yao. Wananchi wanatengeneza mswada wanaupeleka kunakohusika ili kuharakishwa lakini mpaka leo suala hili lipo muda mrefu.

Mhe. Spika, hata sisi Wajumbe wako wa Baraza la Wawakilishi kama hatujapata habari hatuwezi tukazungumza katika chombo hichi. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba sasa hivi wakati umefika ule mswada wa haki ya habari uliopelekwa wizarani kwake sasa hivi kuuharakisha ili kuuleta Barazani na sisi tukaweza kutoa maoni yetu, ili ikawepo sheria katika utawala bora kuhakikisha kwamba kila mwananchi anapotaka kupata habari awe anaipata bila ya vikwazo.

Mhe. Spika, swali (b) tumeshuhudia hivi karibuni serikali ikisema kwamba itaweka Maafisa wa Habari katika kila wizara kwa ajili ya kuweza kutoa habari. Lakini mpaka sasa hivi kuna tatizo wananchi wanapotaka kupata taarifa muhimu ndani ya mawizara sio ambazo zinaingilia ulinzi au usalama wa nchi bado wanakosa kupata hizo habari. Kwa kuwa hakuna hii sheria ambayo inambana mtendaji yeyote kuweza kutoa taarifa yoyote wanayotaka wananchi. Je, kucheleweshe sheria hii hatuoni kwamba tunawanyima haki ya kikatiba wananchi.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza tunaupokea ushauri wake wa kuharakisha ili mswada huu uweze kuja katika chombo hichi kitukufu. Tutaufanyia kazi vizuri ili tuhakikishe kwamba unaletwa hapa Barazani kuweza kujadiliwa na Waheshimiwa Wajumbe ili upitishwe kuwa sheria.

Mhe. Spika, kuhusu swali (b) serikali imetoa utaratibu maalum uliowekwa kwa wizara na taasisi zote za serikali namna ya kutoa taarifa zake kwa taasisi zote za serikali. Hivyo, utaratibu umewekwa na milango yetu iko wazi kutoa taarifa hizo. Mhe. Spika, tunalihakikishia Baraza lako tukufu kwamba utaratibu huu utasaidia sana kuhakikisha wananchi wanapata taarifa kwa wakati.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza kabla sijataka niulize swali langu namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwa jinsi alivyoweza kusaidia kujibu swali langu Nam. 37.

Nam. 47

Uwekezaji uliokwama wa *Agakhan Foundation* Mangapwani

Mhe. Hamza Hassan Juma - Aliuliza**:**

Eneo la Mangapwani limemilikishwa kwa Shirika la *Agakhan Foundation* kwa ajili ya uwekezaji mkubwa wa hoteli ya kitalii na kujenga kiwanja cha mchezo wa *Golf* ambao hupendwa sana duniani hasa na matajiri wakubwa.

(a) Je, Mhe. Waziri, mbona mradi huo kwa muda mrefu umekwama.

(b) Unaweza kutuambia kuna jitihada za kuukwamua mradi huo.

(c) Je, wananchi hasa wa Mangapwani unawaambia nini kuhusu uwekezaji huo ambapo walitegemea kupata ajira katika eneo lao.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo - Alijibu**:**
Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 47 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, mradi kubwa wa uwekezaji wa hoteli ya kitalii na kujenga kiwanja cha mchezo wa *Golf* wa *Agakhan Foundation* hauko katika Wizara yangu. Naomba Mhe. Mwakilishi kuliwasilisha swali lake hilo kwa mamlaka inayohusika ambayo ni *ZIPA*.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwanza nasikitika sana kwa jawabu la Mhe. Waziri. Mhe. Spika, tunavyojua serikali inafanyakazi kwa mashirikiano. Mhe. Spika, swali langu nimelipeleka kwa muda mrefu sana, sasa kama wizara ilikuwa inaona halihusiani lilikuwa lirudishwe tena Barazani na lipelekwe tena katika wizara husika. Leo Mhe. Spika, mimi nashangaa kwamba swali baada ya muda mrefu naliuliza hapa naambiwa niliondoe

nilipeleke katika wizara husika. Mhe. Spika, mimi ninavyojua kwa utaratibu serikali inafanyakazi kwa pamoja na masuala haya mawaziri wanapewa. Mhe. Spika, suala hili linajulikana naomba nipewe jawabu.

Mhe. Spika: Yanapotokea mambo kama haya huwa tunakwenda kwa waziri yule anayehusiana na mambo ya Shughuli za Baraza.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza naomba nikubaliane na Mhe. Mwakilishi ni kweli kwamba serikali inafanyakazi kwa pamoja na ni wajibu wa wizara iliyopelekewa swali hili kulirudisha kwa wizara inayohusika. Mhe. Spika, naomba kulichukua swali hili na kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba kikao kijacho tutahakikisha swali hili limejibiwa na serikali.

Mhe. Spika: Nafikiri hakuna waziri mwengine anayetaka kuongeza kitu. Kwa hiyo, hakuna matayarisho ya majibu nikuombe radhi Mhe. Mwakilishi tusubiri kikao kijacho swali lijibiwe kwa usahihi.

Muongozo wa Spika

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako kuna suala dogo nilikuwa naomba nilizungumze linalohusiana na Haki, Kinga na Fursa za Wajumbe na linahusiana na Azimio ambalo tulilipitisha juzi hapa. Sikusudii kurejesha mjadala juu ya suala hilo nataka nikuhakikishie kabisa.

Lakini Mhe. Spika, tangu Jana kuna baadhi ya vyombo vya habari vimekuwa vikipotosha kwa lile ambalo limepitishwa hapa. Sasa nilikuwa naomba muongozo wako ili utumie kiti chako kidogo kuviambia hivi vyombo vya habari. Inaonekana baadhi ya waandishi wa habari au wengi wao walivyoelewa ni kama vile msingi wa hoja tuliyoipitisha hapa ilikuwa ni kuzungumzia kutoshirikishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzíbar wakati huo haukuwa kabisa msingi wa hoja. Msingi wa hoja ulikuwa ni kitendo kile kwenda kinyume na Azimio la Baraza mwaka 2009.

Sasa Mhe. Spika, nimepata hapa kwa mfano maoni ya mhariri wa gazeti la Mwananchi la leo na inasikitisha kidogo kwa sababu nimelipata katika mtandao maana magazeti huwa yanachelewa kufika hapa. Lakini nimesikitika kwa sababu kwanza limepotosha lakini limeandika maoni ya mhariri ambayo yanazungumza “Kwa upotoshaji huu Ismail Jussa aombe radhi.” Naomba kwa faida ya Baraza kidogo nisome sehemu ndogo tu ya maoni.

Inazungumzia yaani baada ya kutoa ufafanuzi “Hivyo ndivyo Waziri Tibaijuka alivyofanya na tunakubaliana nae kabisa aliposema alilazimika kutoa ufafanuzi

wa kina kwa sababu pande hizo mbili za Muungano hazipaswi kugombea kitu wakati nyumba inayojengwa ni ya wote. Moja ya sababu zilizofanya turidhishwe na ufafanuzi wake ni pale alipotoa ushahidi wa namna Zanzíbar ilivyohusishwa kikamilifu kupitia SMZ katika ngazi zote tangu 2007 kiasi cha kuibua mashaka kama kweli Mwakilishi huyo wa Mji Mkongwe alipeleka hoja hiyo Barazani kwa nia njema au alidhamiria kuwachafua viongozi wa pande hizo mbili za Muungano kwa kupeleka hoja iliyojengwa kwa misingi ya maneno ya mitaani."

Mhe. Spika, yapo mengi lakini nimeambiwa niyaache. Sasa nasema kwanza kanuni au maadili ya vyombo vya habari hutakiwi kutafuta maoni au kuandika *reaction* ya *story* ambayo wewe mwanzo hukuiripoti. Gazeti la Mwananchi halikuripoti kabisa juu ya kadhia iliyotokea Barazani na hoja iliyopitishwa lakini badala yake limekwenda kuandika *reaction* ya waziri aliyeandika. Lakini hiyo isingenishughulisha kwa sababu mimi naamini mwanasiasa huwa anapaswa kuwa na ngozi ngumu na mimi ninayo kabisa ya kuhimili vishindo hivyo.

Lakini nilichosikitika Mhe. Spika, ni huu utaratibu tukiuachia utakuwa unaingilia haki za Baraza hili kwa sababu sasa maoni kama haya yanapotosha kabisa kile ambacho kililetwa Barazani, kilijadiliwa na hatimae kupitishwa. Kwa hakika kwa maelezo yaliyojadiliwa hapa tulikuwa tunajua kwamba Serikali ya Zanzíbar imeshirikishwa, tulichokuwa tunahoji ni kwamba Serikali ya Zanzíbar tulishiriki vipi katika kitu ambacho tayari kulikuwa kuna Azimio la Baraza.

Mhe. Spika, naomba muongozo wako tunafanya nini kwa vyombo vya habari kama hivi na mhariri huyu ambaye anapotosha kabisa maazimio ya Baraza lako tukufu. Mhe. Spika, naomba muongozo wako.

Mhe. Spika: Kabla sijatoa muongozo sijui kama sijalipata sawa sawa kuhusu *issue* ipi hasa.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, moja katika misingi yetu hapa ni kuheshimu majadiliano ambayo yanafanyika hapa na maamuzi ya Baraza na hakuruhusiwi mtu kupotosha maamuzi ya Baraza hili. Lakini ukisoma msingi wa haya maoni na nitakupatia hapa yanajielekeza kama vile kwamba msingi wa hoja tuliyoijadili hapa ni niseme hoja hii isitafutwe tena ya Mhe. Jussa ni hoja ambayo imepitishwa na Baraza yanaonesha kama vile kwamba msingi wa hoja ile ilikuwa ni kudai kwamba Serikali ya Zanzíbar haikushirikishwa wakati huo haukuwa msingi wa hoja.

Mhe. Spika: Kwenye *issue* ya bahari kuu au *issue* gani.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, ilikuwa ni ile hoja ya kuhusu bahari kuu. Samahani kama nilikuwa sikulitaja hilo Mhe. Spika. Nilikuwa nasema ni ile hoja binafsi ambayo tuliijadili hapa siku ya Jumatatu ya bahari kuu. Sasa nikisema msingi wa hoja ambao bahatí nzuri tumeigawa kwa wajumbe wote hapa haikuwa kuhoji kwamba Serikali ya Zanzíbar haikushirikishwa, ilikuwa ni kuhoji hiyo kwamba Serikali ya Zanzíbar kama ilishirikishwa imeshiriki vipi kitendo ambacho kilikuwa kinakwenda kinyume na Azimio la Baraza la mwaka 2009. Sasa sitaki kurejesha huko kwa sababu hilo tumeshalimaliza.

Mhe. Spikla, hoja yangu ni kwamba nataka muongozo wako kwamba kwa mhariri wa gazeti hili ambaye amepotosha na kufika hadi ya kuandika maoni ambayo yanalipotosha suala hili kwa wananchi. Kwa hivyo, nataka kauli yako Mhe. Spika, ili jambo hili liwache kuwapotosha wananchi na viwache kuleta mgongano kwa mambo ambayo hawajayafanyia utafiti wala hawakufanya juhudi ya kujua hasa Baraza hili lilipitisha maamuzi gani na badala yake wanawachanganya wananchi sasa.

Mhe. Spika: Sikupendelea kutoa uwamuzi au muongozo kuhusu gazeti hili na muariri huyo, kwa sababu upo utaratibu, kanuni siikumbuki ipo, lakini upo utaratibu. Kama kuna mhariri amekwenda kinyume na mambo yaliyoamuliwa na amepotosha, basi inaweza ikaja hoja kwamba muhariri huyo atakiwe kuja kutoa maelezo juu ya upotoshaji ule. Pia upo utaratibu wa kuweza hata kuitwa katika Baraza hili. Ili upotoshaji ule aelezwe halafu na yeye apate nafasi ya kujibu kwa nini akafanya vile. Halafu baada ya kueleweka na chombo hiki kikaridhika kwamba kweli amepotosha kwa makusudi, hupewa maelekezo au maagizo ya kufanya masahihisho ama kuna jambo jengine ambalo litaagizwa afanye hivyo.

Kwa hivyo, kutoa au kuagiza maelezo ya moja kwa moja wakati bado hoja hiyo ya mtu yule kuitwa hapa na yeye akajitetea, kidogo inakuwa pana uzito wa kufanya hivyo. Kama unahisi amepotosha mambo na maamuzi yaliyotolewa hapa juu ya hoja ile ambayo ililetwa kupitia kwako mwenyewe, basi unaweza ukaleta hoja hiyo baadae wakati muafaka, kwa sababu na muda wenyewe unayoyomea. Kesho tunategemea kipindi cha asubuhi kufunga mkutano huu baada ya kipindi cha maswali ili mhariri huyo aje apate nafasi na yeye kuweza kujitetea na hatimaye maamuzi muafaka yakaweza kutolewa. Kutoa maagizo moja kwa moja inaweza ikaleta malumbano sasa hata dhidi ya kiti kinachotoa maamuzi hayo kwa sababu hakupata nafasi ya kujitetea.

Kwa hivyo, nielekeze kama jambo hilo limepotosha kwa mujibu ulivyosoma gazeti hilo na kwa kiasi kikubwa imeingilia mwenendo mzuri wa chombo hiki, basi hiyo hoja unaweza ukaileta na hatimaye akaitwa mtu huyo, ili tukatoa maamuzi na yeye akawa amepata nafasi ya kujitetea.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika. Mhe. Spika, nadhani unanielewa kwa jinsi ninavyokiheshimu kiti chako na maelekezo yako, kwa hivyo nalikubali. Mhe. Spika, kwa faida ya wajumbe tu nataka niseme kwamba katika sheria hii ya *powers, privilege and minutes* za wajumbe, kifungu cha 32(1) kinasema;

Kifungu cha 32(1)

> "*Any person who:-*
> *(a) publishes any false or scandalous libel on the house or any Committee which Willfully misrepresents in any way proceedings of the house or any Committee*;
>
> Halafu yanaendelea makosa mengine. Lakini mwisho inamaliza pale.
>
> "*Commits an offence and shall on conviction be liable to a fine not less than three hundred thousand shillings or to imprisonment for a term not exceeding three years or to both such fine and imprisonment".*

Sasa nimeelewa muongozo wako na mimi nilikuwa naomba basi kwa kutumia kiti chako, wala sina lazima kwamba lifanyike leo ama kesho, kwa sababu hoja yangu iko hapa katika ku-*miss represent* yale ambayo tulileta hoja hapa na tuliamua. Kwa hivyo, naomba kwamba Baraza lifanye utaratibu wa kumtaka mhariri aje athibitishe haya aliyoyaandika, halafu hizo habari nyengine zitafuata baadae Mhe. Spika.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Ahsante sana Mhe. Spika, Mhe. Ismail Jussa kama alivyotangulia kusema mwanzo kwamba alitaka muongozo wako. Mhe. Spika, kama mwenyewe alivyotangulia kusema na mimi pia nimuunge mkono kwamba nimeridhika kabisa na muongozo ambao umeutoa, kwamba kama tunataka Baraza lichukuwe hatua, Majadiliano ya Baraza yanaanzishwa kwa hoja.

Kwa hivyo, iletwe hoja ya kuhusiana na suala hili, halafu Baraza litatoa uwamuzi. Kama suala ni *offence* Baraza hili halitowi hukumu ya *offence* hilo litafuata baada ya hatua zitakazoonekana na Baraza hili kuchukuliwa. Lakini kama ni Baraza hili kutoa uwamuzi, mimi nadhani Mhe. Spika, umetoa muongozo mzuri na sikutegemea kama utahitaji maelezo ya ziada kwamba iletwe hoja baadae hoja hiyo itaamuliwa na Baraza hili.

Mhe. Spika: Basi nafikiri tunaweza tukajenga mashirikiano kati ya Mhe. Mjumbe, Ofisi ya Mhe. Mwanasheria Mkuu hapa na hata Ofisi ya Makamu wa

Pili wa Rais ambaye ndiye dhamana wa shughuli za humu ndani. Tuone nini kitakachofuata baadae, tukiona jambo hilo lina uzito wa kiasi hicho cha kuchukua hatua hizo.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru sana kwa hekima na busara zako zinazoogelea katika bahari hii. Lakini Baraza lako tukufu Redio FM na mwandishi mmoja wa kike aliiandika makala ya redio na wajumbe wa ndani ya Baraza wakachangia hoja ile, sio hoja lakini ni kama hivi leo mtu akasema kuwa imepotoshwa. Hujataka Baraza mjumbe alete hoja, tulisikiliza na tukataka sasa yule mwandishi kwa hekima na busara Ofisi ya Baraza imuandikie na zipo kumbukumbu. Tungejua suala hili mapema basi tungekuja na kumbukumbu, lakini kama jioni ipo au kesho tutakuja nazo. Kwa sababu Mhe. Spika, tumeshajenga kustahamiliana na vyombo vya habari. Tumeshaondoka wakati ule wa hasia na mabavu na kadhalika. Hoja imetolewa na maelezo yameelezewa.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza Hassan Juma amenikumbusha hapa kwamba tuliwahi kutoa adhabu tulimfungia mwandishi wa kike na yule kijana wa kiume nimemsahau jina lake, na yeye alitoa maelezo. Sasa nafikiri Mhe. Spika, ya kufika kwenye hoja hiyo, hebu tutizame Hansard tustahamili mpaka kesho, utizame kumbukumbu zako na halafu tuone nini tufanye ili tuweze kuridhisha hali.

Mhe. Spika, kuna mtu mmoja aliniambia jana kwamba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kila mmoja atowe Shs. 100,000/= tununuwe ng'ombe tuchinje mlangoni, kwa sababu Baraza limechafuka, nikamwambia hapana haina haja.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, ulimtaka Mhe. Mwanasheria Mkuu atowe mawazo. Lakini sisi tulikuwepo hapa Mhe. Spika, vipindi vya nyuma. Nafikiri tu utumie hekima yako na busara yako, ili tuje tutizame kumbukumbu zinasema nini, ni jambo dogo tu kapotosha tu. Nafikiri Mhe. Spika, umenielewa, ahsante sana.

Mhe. Spika: Nafikiri mashauri na maelekezo uliyoyatoa yatasaidia kuona haja hiyo ambayo Mhe. Mjumbe amesisitiza. Kwa hivyo, nadhani tufuate ushauri huo kwa pamoja ili tuone jambo hili kisheria tunaweza tukafanyaje.

Waheshimiwa Wajumbe, nawashukuru nafikiri baada ya hapo sasa tuendelee.

KAULI ZA MAWAZIRI

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kuwasilisha taarifa rasmi kuhusu hitilafu za kiufundi kwa vyombo vya baharini siku za hivi karibuni.

Mhe. Spika, utakumbuka kwamba tarehe 24/07/2011 niliwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu hili taarifa juu ya hitilafu za kiufundi kwa vyombo vya baharini siku za hivi karibuni kama kauli ya waziri.

Mhe. Spika, mara baada ya uwasilishaji huo, baadhi ya wajumbe walipata fursa ya kuchangia taarifa hiyo kwa kuuliza maswali, kuhoji, kutoa ushauri na kutaka ufafanuzi kwa mambo kadhaa.

Aidha, na mimi ulinipa fursa ya kujibu na kufafanua baadhi ya masuala na hoja mbali mbali za wajumbe wa Baraza lako hili tukufu. Mhe. Spika, wakati naendelea kufanya hivyo kwa madhumuni ya kuhitimisha uwasilishaji wa taarifa yangu, ndipo wewe Mhe. Spika, ulipotoa maelekezo yako ya hekima na ya busara kabisa na uliagiza mambo yafuatayo.

1. Kutoa muda wa kuifanyia kazi taarifa hii ili kuifanya bora zaidi.
2. Kuileta taarifa hii kwenye kikao kijacho.

Mhe. Spika, taarifa hii ilikuwa iletwe katika kikao cha mwezi wa Oktoba, 2011. Mhe. Spika, sasa ni kipindi kirefu tangu ilipotolewa taarifa hii na ulipotoa maelekezo hayo.

Mhe. Spika, masuala na hoja za wajumbe waliochangia nyingi zilishabihiana, hivyo maelezo yaliomo katika taarifa hii hayajibu swali la mjumbe mmoja mmoja, lakini inajibu maswali yote na kufafanua kwa kiasi kubwa.

Mhe. Spika, taarifa hii ni utekelezaji wa maagizo yako uliyoyatoa kama ifuatavyo.

Kuhusu suala la ununuzi wa meli mpya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano, ikishirikiana na Wizara ya Fedha, Uchimi na Mipango ya Maendeleo, zimeagizwa na serikali kuu kutafuta fedha kwa ajili ya ununuzi wa meli mpya. Aidha, wizara hizi zinaendea kufanya mazungumzo na wawekezaji mbali mbali ili kuangalia uwezekano wa kuwekeza katika kupata meli mpya kwa njia ya ubia au mkopo.

Mhe. Spika, hadi sasa wizara imekutana na kampuni mbali mbali kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo na kampuni zenyewe ni hizi zifuatazo:-

1. Sultan Farmal International ya Sudan
2. YEA Horizonto
3. Kampuni za Uturuki
4. Al Yussuf Charitable Society ya Saudi Arabia na
5. Demonias ya Uholanzi

Mapendekezo yaliyotolewa na wizara hizo yanafanyiwa kazi ili yaweze kupelekwa serikalini kwa maamuzi.

Mhe. Spika, vile vile Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imezitumia kampuni mbali mbali zinazojishughulisha na utengenezaji wa meli ship bilders vigezo na sifa za aina ya meli ambayo serikali inakusudia kununua kwa ajili ya abiria mizigo na abiria na mafuta. Hizo ni namna tatu za meli. Ili kupata makisio ya gharama muda wa ujenzi na mambo mengine yanayohusiana na taratibu za kupatikana kwa meli hizo. Kampuni hizo ni;

1. Kampuni za Japan
2. China
3. Korea
4. Uturuki
5. Sweden
6. Afrika ya Kusini

Haya yalikuwa ni maagizo ya serikali kuu kuwapelekea wajenzi wa meli kwa zile nchi ambazo tunaona kabisa wana umaarufu huu na hatua hiyo imeshachukuliwa.

Mhe. Spika, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pia imo katika hatua za mwisho za kuandaa waraka kwa ajili ya wawekezaji katika usafiri wa majini. Viongozi wakuu wa serikali kila wanapokutana na mabalozi na washirika wa maendeleo wanakuwa wakizungumza juu ya uwezekano wa kuipatia serikali meli kwa ajili ya kuondoa tatizo la usafiri na usafirishaji kwa Zanzibar.

Mhe. Spika, hizi ni juhudi ambazo Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Serikali Kuu kwa kupitia viongozi wake wakuu wa juu zinafanyika.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kanuni na udhibiti wa meli chakavu. Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inakamilisha kanuni za sheria nambari 3 ya mwaka 2009 iliyounda mamlaka ya usafiri baharini ambayo itaweka pamoja na mambo mengine umri wa meli itakayoruhusiwa kuingizwa nchini.

Mhe. Spika, kuhusu suala la uokozi, hili ni suala la kitaifa ambalo linategemea taasisi mbali mbali za serikali na za kibinafsi. Hata hivyo, linapotokea tukio kama hilo hatua za haraka kuvishajihisha vyombo mbali mbali vya baharini na angani kwa ajili ya uokozi. Aidha, serikali huomba msaada unaohitajika katika taasisi za ndani na nje ya nchi kwa kazi ya uokozi. Kuhusu kuahirishwa kwa safari za mara kwa mara kwa vyombo vya baharini. Kiutaratibu Mhe. Spika, haitakiwi kufanya hivyo, ila kwa sababu maalum za msingi pindipo ikitokezea kuahirishwa kwa safari bila ya sababu hizo basi vyombo hivyo hutozwa faini.

Mhe. Spika, kuhusu utoaji wa taarifa za mamlaka ya hali ya hewa ni kwamba taarifa hutolewa kila siku na Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa kupitia televisheni na redio TBC. Hivyo tunawashauri wenye vyombo na wananchi kwa jumla kufuatilia na kusikiliza taarifa hizo. Aidha, mamlaka baada ya kupata taarifa hizo za hali ya hewa, basi huziwasilisha taarifa hizo kwa manahodha pamoja na wamiliki wa meli kabla ya kuanza safari zao.

Kuhusu suala la uingiaji wa abiria na upakiaji wa mizigo, maofisa kutoka taasisi mbali mbali zikiwemo ZMA, ZRB, Bandari, Polisi, KMKM na Usalama wa Taifa wanakuwepo milangoni wakati wa kupanda na kushuka abiria kwa ajili ya kudhibiti usalama na idadi ya abiria, mapato kwa wanaoingia na kushuka melini.

Mhe. Spika, ukaguzi wa vyombo vya baharini unafuata kanuni na taratibu za kimataifa za Shirika la *International Maritime Organization (IMO)* ambapo meli hukaguliwa kila baada ya miezi mitatu na ukaguzi wa kina hufanywa kila baada ya mwaka mmoja. Aidha, ukaguzi wa chini ya meli kwa meli ambazo wakati meli inaelea hazipatikani kufanyiwa ukaguzi. Meli hizo hufanyiwa ukaguzi kila baada ya miezi 18 kwa kupelekwa chelezoni na vile vile ukaguzi wa shaka hufanywa inapotokezea hitilafu au mamlaka husika inapotilia shaka uzima wa chombo hicho.

Mhe. Spika, meli za abiria zinapaswa kuchukua abiria kwa mujibu wa idadi ya abiriwa iliyopangiwa. Hata hivyo, kumekuwa na tatizo hasa kwa abiria wanaokwenda na kurudi Pemba. Hatua zinachukuliwa kwa mashirikiano ya *Zanzibar Maritime Authority*, Mamlaka ya Usafiri Baharini, wamiliki wa meli ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa suala hili.

Mhe. Spika, serikali ina mpango wa kuliimarisha Shirika la Bandari, ili kuhakikisha kwamba chelezo kinapatiwa vifaa na wataalamu pamoja na nyenzo zinazostahiki kuhakikisha kuwa vyombo vinavyopelekwa katika chelezo hicho vinahudumiwa kama inavyokusudiwa.

Mhe. Spika, kuhusu utaratibu wa safari za Pemba na Tanga, utaratibu hauna tofauti na utaratibu wa safari ya Unguja na Pemba au Unguja na Dar es Salaam. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa sasa haina mpango wa kutafuta boti ndogo kwa ajili ya usafiri wa visiwa vyetu vidogo vidogo vya ndani. Hata hivyo, serikali inakaribisha na inashajihisha wawekezaji binafsi kuwekeza katika maeneo hayo.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nataka kuwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu, kwa michango yao adhimu waliyoitoa kwa njia mbali mbali, lakini yote imesaidia serikali na Wizara ya

Miundombinu na Mawasiliano, pamoja na Mamlaka ya Usafiri Baharini katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA MAWASILIANO NA UJENZI KUHUSU HITILAFU ZA KIUFUNDI KWA VYOMBO VYA BAHARINI SIKU ZA HIVI KARIBUNI

Mhe. Rashid Seif Suleiman: (Kny: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu na Mawasiliano): Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, naomba kutoa hotuba ya Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, kuhusu hitilafu za kiufundi kwa vyombo vya baharini siku za hivi karibuni kwa ripoti aliyoiwasilisha Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Spika, kwanza kabisa tunapenda kuipongeza serikali kwa uamuzi wake wa kuunda Tume maalum kuchunguza kadhia ya ajali iliyoihusisha meli ya Mv Spice Islander 1, ambapo ripoti ya Tume hiyo imetolewa kwa umma wa Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla hivi karibuni. Kwa jinsi ripoti ya Tume hiyo ilivyotolewa, Kamati yetu imeshawishika kuamini kuwa Tume ilifanya kazi zake kwa uhuru na utaalamu walionao wajumbe wake bila ya kuingiliwa na serikali. Kamati inapenda kuipongeza serikali kwa hilo. Hatimaye baada ya ripoti hiyo, tumeona jinsi Serikali ilivyodhamiria kutekeleza mapendekezo ya Tume hiyo ya wataalamu. Ni imani yetu kuwa serikali itatekeleza mapendekezo mengine yaliyomo katika ripoti hiyo ya Tume likiwemo la uimarishaji wa Mamlaka ya usafiri baharini ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mkubwa.

Mhe. Spika, katika kauli ya waziri aliyoiwasilisha katika Baraza lako tukufu, Mhe. Waziri ameeleza juu ya hatua mbali mbali zilizochukuliwa katika kuhakikisha kuwa serikali inapata meli ya uhakika itakayosaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la usafiri wa baharini hasa baina ya Unguja na Pemba.

Tangu Mhe. Waziri alipotoa kauli kuhusiana na masuala haya kwa mara ya kwanza mnamo mwezi wa Julai 2011, takriban miezi sita imeshapita. Tangu ajali ambayo ilihusisha meli ya Mv Spice Islander 1 na kugharimu maisha ya mamia ya watu itokee, ni kiasi ya miezi mitatu sasa imeshapita.

Mhe. Spika, Kamati yetu inasikitika kuona kuwa kauli hii ya Mhe. Waziri haitoi matumaini kuwa suala hili la kupatikana kwa meli hiyo litapatiwa ufumbuzi hivi karibuni. Kamati inarejea kauli yake ya kuiomba wizara na

serikali kwa ujumla, kulipa kipaumbele suala la ununuzi wa meli ama kwa njia ya moja kwa moja au kwa njia ya mkopo ili kuweza kupunguza tatizo la usafiri kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, Kamati yetu inafahamu kuwa ununuzi wa meli ni mradi mkubwa unaohitaji fedha nyingi. Hata hivyo, tunaamini kwamba kukiwepo na umakini katika suala hili, dhamira ya dhati, mipango mizuri na ufuatiliaji wa karibu pamoja na kuweka kipaumbele katika suala hili, tunaweza kuifikia azma ya ununuzi wa meli hiyo katika muda si mrefu ujao.

Mhe. Spika, katika kauli ya waziri suala la uingiaji abiria na upakiaji mizigo limeelezwa, ingawa kwa maoni ya kamati suala hili halikuelezwa hasa kwa uzito unaostahili kwa kuzingatia kuwa nchi yetu ilikumbwa na msiba mkubwa wa ajali ya meli, iliyogharimu maisha ya watu wengi ambayo inaaminika ilitokana kwa kiasi kikubwa na kupakia abiria na mizigo kuliko uwezo wa chombo husika.

Kauli hiyo ya Waziri inaeleza tu kuwa, maofisa kutoka taasisi kama Mamlaka ya Usafiri Baharini, Shirika la Bandari, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato Zanzibar na Idara ya Usalama wa Taifa wanakuwepo milangoni kwa madhumuni ya kudhibiti usalama, idadi ya abiria na mapato.

Mhe. Spika, kauli hiyo ya waziri inaonekana kuegemea katika nadharia kuliko kuzingatia uhalisia na uzito wa tatizo hili la upakiaji wa abiria na mizigo kupindukia uwezo wa vyombo vinavyohusika. Kamati yetu ilitarajia kuona katika kauli hiyo mikakati madhubuti inayoonyesha namna ya kumaliza tatizo hilo la ujazaji wa abiria na mizigo kupita kiasi kilichoruhusiwa, hasa baada ya ajali kubwa ya meli iliyotokea hivi karibuni.

Mhe. Spika, kamati yetu inaendelea kutoa msisitizo mkubwa kwa Wizara ya Miundombinu na taasisi zote zinazohusika na usimamizi wa upakiaji wa abiria na mizigo, kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria na kuthamini maisha na mali za wananchi, badala ya kuhatarisha maisha ya wananchi hao kwa kutozisimamia vyema taratibu za upakiaji wa abiria na mizigo.

Kutokana na uzito wa suala hili na athari ambazo tumeshazipata kutokana na kukosa umakini katika usimamizi wa upakiaji abiria na mizigo, kuna haja kwa viongozi wa wizara na taasisi husika kufuatilia kwa ukaribu zaidi na kuchukua hatua madhubuti kwa wote wanaozembea katika kusimamia suala hili, badala ya viongozi hao kukaa ofisini na kupokea ripoti zisizo na ukweli.

Mhe. Spika, kamati yetu inashauri wizara kuupitia mfumo wa upakiaji abiria katika ndege, ambao kwa namna yoyote hautoi nafasi kwa wamiliki na

waendeshaji wa mashirika ya ndege kuongeza idadi ya abiria kuliko uwezo halisi wa ndege hizo, ili kuona kwa namna gani na kwa kiasi gani unavyoweza kuutumia katika usafiri wa baharini na kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza.

Mhe. Spika, kauli ya Waziri pia inaeleza kwa ufupi kuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inakamilisha Kanuni ya Sheria Nam. 3 ya Mwaka 2009, Sheria ya Mamlaka ya Usafiri wa Baharini, kanuni ambayo kwa mujibu wa kauli hiyo ya waziri, itaweka ukomo wa umri wa meli na vyombo vyengine vya usafiri vitakavyoruhusiwa kuingizwa nchini. Kuwepo kwa kanuni hizo zitakazodhibiti uingizaji wa vyombo vya usafiri wa baharini ni suala muhimu sana ili kunusuru athari zaidi zinazoweza kujitokeza iwapo tutaendelea kukosa taratibu madhubuti za kusimamia suala hili na hivyo kutoa mwanya kwa vyombo vya usafiri vikongwe sana, kuingizwa na kutoa huduma za usafiri hapa nchini.

Mhe. Spika, hata hivyo, kamati yetu inahisi kuwa suala hili lilipaswa kufanyiwa kazi kwa haraka zaidi, toka Kamati hii pamoja na Wajumbe wa Baraza walipoitanabahisha Wizara juu ya umuhimu wa kuzifanyia kazi kanuni hizo ili pamoja na mambo mengine kudhibiti uingizaji wa vyombo vya usafiri baharini katika Mkutano wa bajeti mnamo mwezi Julai, 2011. Kwa mnasaba huo, kamati inaendelea kusisitiza kuwa kanuni hizo zifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo kwa madhumuni ya kuhakikisha kuwa vyombo vinavyoingizwa nchini kwa ajili ya kutoa huduma za usafiri wa baharini vinakuwa katika hali ya kuridhisha.

Mhe. Spika, pamoja na ukweli kuwa tumekuwa na sheria na kanuni nyingi zinazosimamia masuala mbali mbali, kumekuwa na tatizo kubwa la usimamizi mzuri wa sheria na kanuni hizo. Hivyo, ni vyema Wizara ikazisimamia kwa umakini mkubwa kanuni hizo badala ya kubakia katika maandiko tu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Abdalla Juma Abadalla: Ahsante Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Pili naipongeza sana serikali kwa namna ya hatua ilizochukua katika kushughulikia ajali ile ya meli na namna walivyojidhatiti katika katika kutatua tatizo la usafiri.

Mhe. Spika, wali langu ni moja. Tukiangalia ukurasa wa tatu wa taarifa hii ya Mhe. Waziri ameeleza kwamba katika kipindi cha miezi kumi na nane, basi meli zinazosafirisha abiria huwa zinafanyiwa ukaguzi kule chini ambako katika ukaguzi wa kawaida huwa hakupatikani.

Sasa mimi nauliza meli yetu ya MV. Serengeti ambayo ni mashuhuri sana kwa kusafirisha abiria kati ya Unguja na Pemba.

(a) Hivi mara ya mwisho meli ilifanyiwa mwezi gani?

(b) Ripoti hiyo ya ukaguzi inaelezea vipi kuhusu uzima wa meli hiyo?

Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwanza sina budi kuipongeza serikali ambayo iliunda tume. Kwa kweli nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambaye aliunda tume kwa makini, kwa sababu hawakutiwa watu holela kama tunavyozoea siku zote. *(Makofi)*

Lakini na mimi ninalo swali kwamba katika ripoti ya Mhe. Waziri ameeleza hapa ni kampuni tofauti ambazo serikali inashirikiana nao.

Je, haoni kwamba kuna haja ya kumtumia mzaliwa mwenzetu wa hapa Zanzibar, ambaye ni Said Salum Bakhresa na nina hakika uwezo anao, kuliko kukimbilia makampuni ya nje, kwa ajili ya kumshawishi kuwa na yeye ni miongoni mwa watu wanaoweza kufanya miujiza. Lakini tumezoea kukimbilia wafadhili wa nje. Kwa hivyo, naomba tumtumia mwananchi mwenzetu ambaye amejitolea kwa vyombo vyote.

Ahsante Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, na mimi nishukuru kupata nafasi hii. Nianze kwa kuipongeza serikali pamoja na Tume Maalum iliyoundwa kwa ajili ya uchunguzi wa kuzama kwa Meli ya *MV. Spice Islander I. (Makofi)*

Kwa kweli tumekuwa na matumaini mazuri juu ya kazi ya kamati ile na hata ripoti iliyotolewa. Kutokana na hali hiyo, hatuna budi kuipongeza serikali, hasa ambapo tumeona taarifa imeanza kufanyiwakazi. Vile vile naamini uongozi utaendelea kuifanyiakazi zaidi, ili hatimaye haki ipatikane kwa wale ambao wameathirika na suala hili. *(Makofi)*

Mhe. Spika, kutokana na uzito wa suala hili, haja yetu ilikuwa tuijadili ripoti hii. Lakini kwa kuwa leo umetuambia tuulize maswali, mimi naheshimu sana kiti chako na nitafanya kama ulivyoagiza. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ukweli bado tunalo tatizo kubwa katika suala hili la usafiri wa baharini, licha ya serikali kudhihirisha kwamba bado iko mbioni, maana mbio za serikali hatuzijui lini zitafikia ukomo. *(Makofi)*

Kwa kweli bado matatizo yanaendelea kama vile matatizo ya ulanguzi wa tiketi, vyombo kuahirisha safari, abiria kujazwa pamoja na uchakavu wa meli. Hata hivyo, kwa sababu Mhe. Spika, umetaka tuulize maswali basi mimi nitauliza swali moja tu.

Mhe. Spika, tulikwenda Shirika la Meli chini ya uongozi wa *Professor* kama Mwenyekiti wa Bodi wa Shirika la Meli Alhajj mzee wetu Mhe. Ali Mzee Ali, basi shirika limefanya juhudi kubwa ya kutafuta meli mpya, tena ya kisasa ya abiria na mizigo na yenye kwenda kwa kasi walitafuta nchini Afrika ya Kusini kule na tayari wameshakubaliwa kila kitu.

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi ilitakiwa idhamini mkopo, yaani kazi yake ilitakiwa idhamini mkopo, lakini wao wenyewe walikuwa wako tayari na kila kitu kimeshapangwa.

Sasa namuomba Mhe. Waziri au serikali kwa jumla itueleze ni sababu zipi zilizopelekea serikali kutokubali kudhamini deni lile. Kitu ambacho kingepelekea hivi sasa kuepuka na haya mambo ya kuambiwa tunapewa Uturuki, Mwanza au wapi, ingekuwa mambo yameshamalizika na hivi sasa tunayo meli mpya tena ya kisasa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, ni sababu zipi zilizopelekea serikali kukataa kitu ambacho tayari kwa asilimia kubwa tunacho mikononi tena kwa mkopo wenye masharti nafuu, kulikoni hivi sasa kuanza kazi upya kwenda kutafuta meli? *(Makofi)*

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante. *(Makofi)*
Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi niendelee kuipongeza serikali kwa kuweza kutuletea ripoti nzuri kwa kweli imekuwa makini katika hili. Kwa hivyo, mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Wawi naipongeza sana serikali kwa kazi nzuri iliyofanya ya kutuletea ripoti. *(Makofi)*

Mhe. Spika, Pemba kwenda Tanga usafiri wao mkubwa wanatumia vyombo vya usafiri wa bahari. Kwa kweli tunaishukuru serikali kwa kuingiza *program* kwamba bodi hizi ndogo ndogo zinakwenda, lakini kutoka Pemba kwenda Tanga hakuna usafiri, isipokuwa MV. Nura ambayo ni meli ndogo sana, jambo ambalo ni tatizo kubwa kwa wasafiri wa Pemba kwenda Tanga. *(Makofi)*

Kwa hivyo, nadhani mpango wa serikali wa kununua meli inaonekana ni wa muda mrefu. Je, ni lini serikali itawawekea wasafiri wanaokwenda na kurudi baina ya Pemba na Tanga, vyombo vya uhakika kama walivyosanya hivi sasa kutoka Pemba Unguja na Unguja Dar-esalaam. Sasa ni lini watawashawishi hawa wenye bodi hizi za kisasa wafanye safari hizo? Hilo la kwanza.

Pili sitaki nikiuke ile Kanuni ya 58(4), kwa sababu kuna kesi ambazo ziko Mahakamani zinazohusiana na kuzama kwa meli ya *MV. Spice Islander I*. Lakini naomba kuuliza swali moja ni Mhe. Spika katika hili, kwamba kuna mashirika pamoja na taasisi mbali mbali za kimataifa ambazo zilichangia wakati meli ya *MV. Spice Islander I* ilipopata ajali.

Lakini hadi leo hii wananchi wengi wanatuuliza sisi kwamba fedha hizi zitatumika kwa ajili ya kununulia meli nyengine ya kisasa kubwa au tutaletewa sisi wafiwa. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atupe taarifa kuhusu hizi fedha zilizochangwa ambacho ni nyingi sana, yaani mamilioni na wala hatujapata taarifa zake. *(Makofi)*

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura, nikushukuru kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza maswali machache katika ripoti hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, tunajua katika miongozo uliyotoa kwenye Baraza lililopita, yaani ulitoa muongozo wa kuletewa ripoti hii ambayo tunashukuru Mhe. Waziri leo ametuletea. Vile vile kulikuwa na ripoti nyengine iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhusu Ripoti ya Maafa na kamati yangu ilijaribu kutoa maoni.

Lakini baadaye kwa ushauri wa serikali kiti chako kilikubali kwamba ripoti ile isijadiliwe kwa sababu tayari kulikuwa kuna tume ambayo Mhe. Rais aliiunda kwa ajili ya kuchunguza ajali ile, ili Waheshimiwa Wajumbe wasijewakaingilia mamlaka au tume kulazimishwa kufuata hoja za Waheshimiwa Wajumbe.

(a) Sasa swali langu la mwanzo lipo hapa. Je, ukiacha ripoti hii na kwa kuwa hivi sasa tume imeshawasilisha ripoti yake serikalini, hivi waraka ule utaweza kujadiliwa tena hapa Barazani? *(Makofi)*

(b) Mhe. Spika, tulikuwa tunauliza na tunashukuru serikali imetoa ripoti, lakini kwa kuwa sisi ni wawakilishi wa wananchi kupitia majimbo mbali mbali ya uchaguzi na wala si rahisi wananchi wetu hasa walioko vijijini kuweza kupata ripoti ile.

Je, serikali haikuona haja ripoti ile kugaiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi, ili tunapokwenda majimboni kwetu hasa kwa wale ambao hawajui kusoma na kuandika tukaweza kuwasomea na sisi wenyewe kuijua, kwa ajili ya kuwapa nini serikali ilichokiamua? *(Makofi)*

(c) Mhe. Spika, katika ajali ile ya meli ya *MV. Spice Islander I*, tunashukuru watu wengi walichangia na kuna benki ambazo zilitoa ahadi ya kuwachukua au kuwasomesha watoto mayatima ambao waliowachwa na marehemu waliofariki katika ajali ile.

Je, mpaka leo tunaona kimya na wale watoto mayatima wapo na wengine wanapata tabu katika kusoma, hivi serikali suala hili imelichukuliaje. Kwa kweli hasa wale waliokuwa wakitoa fedha zao walikuwa wakieleza wazi wazi kwamba mimi benki yangu itasomesha baadhi ya watoto ambao watakaokuwa mayatima walioachwa na marehemu katika ajili hii.

Mhe. Spika, nije katika ripoti yenyewe kwenye ukurasa wa 3 wa ripoti *paragraph* ya pili ilipoanza hapa Mhe. Spika kuhusu utoaji wa Taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa na kuja kwenye *paragraph* ya chini yake.

Ripoti ya Mhe. Waziri ukurasa wa tatu *paragraph* ya pili inaeleza hivi:-

> "Mhe. Waziri ameeleza kuhusu suala la uingiaji wa abiria na upakiaji wa mizigo maafisa kutoka taasisi mbali mbali zikiwemo ZMA, Bandari, Polisi, *ZRB* na Usalama wa Taifa wanakuwepo mlangoni wakati wa kupanda na kushuka abiria, kwa ajili ya kudhibiti usalama wa idadi ya abiria pamoja na mapato yanayoingia na kushuka melini".

Mhe. Spika, hapa ndipo tunapopata tabu sana na Ripoti au Kauli za Mawaziri wetu, inaweza kufika pahala Mhe. Spika Kauli za Mawaziri wetu wananchi watakuwa wanazidharau, kwa sababu kauli zinakuwa ni nzuri, lakini inakuja katika utekelezaji na usimamizi wa kauli hizi.

Kwa kweli Mhe. Spika, hii *paragraph* niliyoisoma hapa ni maneno mazuri sana, lakini je kama wizara iliwajibika vipi kwa haya ambayo waliyayaeleza wao wenyewe ukiacha ile tume yenyewe, kwa sababu tayari taratibu zinaeleza.

Mhe. Spika, katika kikao kilichopita haya yote tuliyazungumza na kwa bahati mbaya watendaji wa wizara inapokuja bajeti yao wote wanakuwepo pale juu

kwa ajili kusikiliza yale ambayo tunayoyasema. Kwa hivyo, hapa Mhe. Spika, inaonesha ni jinsi gani Baraza lako tukufu la Wawakilishi linavyodharauliwa na watendaji. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Spika, nadhani kifungu cha 43(3) ambapo kauli hii imetolewa na Mhe. Spika, umetoa muongozo vizuri, kwamba haki iliopo ni kuuliza maswali kwa nia ya kufahamu vizuri hii taarifa, hivyo si mjadala wala malumbano.

Sasa nadhani Mhe. Mjumbe anapotoa mchango au mjadala nafikiri ni kinyume na utaratibu ulioelezwa chini ya kifungu cha 43(3). Kwa hivyo, tubakie kwenye maswali, ili tutimize na tufuate Kanuni zetu za Baraza. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Mhe. Mwanasheria Mkuu, nakushukuru kwa kutusaidia kusisitiza kusimamia Kanuni.

Mhe. Hamza Hassan Juma, endelea kuuliza maswali kwa kifupi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, ndio maana mwanzo nilitanguliza ile je, ile Ripoti ya Maafa iliyowasilishwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, lakini nafikiri jawabu yake baadaye nitaipata.

Sasa nakuja kwenye maswali. Je, Mhe. Spika, katika *paragraph* hii ambayo niliyoisoma ukiacha hatua za Mahakama, serikali katika kuwaajibisha wale wote ambao waliohusika mpaka hivi sasa imeshachukua hatua gani, hasa ukizingatia maamuzi ya Mahakama na kwa kuwa watu wenye uwezo wao, inaweza kuchukua zaidi ya miaka mitano pengine maamuzi yale hayajafanyika. Je, maamuzi ya kisiasa ukiacha yale ya Mahakamani, serikali inachukua hatua gani? *(Makofi)*

Mhe. Spika, kwenye *paragraph* inayoendelea naomba kunukuu.

> Katika Ripoti ya Mhe. Waziri ukurasa wa tatu *paragraph* ya nne inaeleza hivi:-
>
> > “Ukaguzi wa Vyombo vya Habarini unafuata Kanuni na Utaratibu wa Kimataifa za Shirika la *IMO*, ambapo meli hukaguliwa mara kwa mara kila baada ya miezi mitatu na ukaguzi wa kina hufanywa kila baada ya mwaka mmoja. Aidha ukaguzi chini ya meli kwa meli ambazo zinaelea hazipatikani kufanywa wakati meli inaendelea na safari zake.

Mhe. Spika, hapa nataka niulize swali. Je, kwa kuwa hizi Kanuni za Kimataifa, ambapo *IMO* ndio inaongoza kwamba meli zinatakiwa kufanyiwa ukaguzi. Je, katika ile meli ambayo iliyopata ajali ilifanyiwa hizi taratibu na kama hazikufanywa hatua gani za kinidhamu zitachukuliwa kwa wale waohusika?

Mwisho kabisa Mhe. Spika, nataka niisome *paragraph* ya mwisho, naomba kunukuu.

Ripoti ya Mhe. Waziri *paragraph* ya mwisho inaeleza hivi:-

> "Mhe. Spika, mwisho kabisa nataka niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao adhimu waliyoitoa kwa njia mbali mbali, lakini yote yamesaidia serikali, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Mamlaka ya Usafiri Baharini katika kutekeleza majukumu yake".

Swali langu lipo hapa. Mhe. Spika, baada ya shukurani za Mhe. Waziri kutupongeza kwa maoni tuliyoyatoa, lakini matokezeo yake maoni yale tuliyoyatoa baada ya kudharauliwa na wizara ndio maana ikatokezea ile ajali. Je, hatua gani msimamizi wa hii wizara zitachukuliwa na serikali.

Mhe. Suleiman Hemed Khamis: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia katika taarifa ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, tunakubali au tunajua sote kwamba baada ya Meli ya *MV. Spice Isander I* kupata ajali na kufariki watu wengi katika ajali ile, ilitolewa michango mingi sana na kupelekwa serikalini kutoka kwenye makampuni na watu binafsi.

Sasa tunataka kujua kwanza ni kiasi gani fedha zote kwa jumla zilipatikana na baada ya kupatikana fedha hizo madhumuni yake hasa nini au zile shilingi 100,000/= zilizotolewa kwa watu ndio mwisho wa safari? Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Pili tunajua sote kwamba hivi sasa tunakabiliwa na nyakati mbili za safari ambazo ni nguvu kutoka Unguja kwenda Pemba. Kwanza kwa hali ya hewa wakati wa kaskazi pamoja na hali ya hewa wakati wa upepo wa kusi.

Mhe. Spika, tunaamini sote kwa jumla kwamba vyombo tulivyonavyo vya *speed boat* kutoka Pemba kuja Unguja au kutoka Unguja kwenda Pemba sasa vinashindwa kuweza kufanya safari. Vile vile tunaamini na tunajua sote kuwa mara nyingi bodi hizi zinakwenda njiani na baadaye zinarudi katika safari yake.

Kwa hivyo, naomba kuuliza ni lini hasa wananchi watapatiwa hiyo meli yao ya haraka, kwa sababu wananchi wanasema kwamba boti hizi kwa safari ya Pemba na Unguja hazitufai. Sasa ni lini hasa tutaweza kupata boti au meli kubwa, ambayo itaweza kuchukua abiria wengi pamoja na mizigo yao.

Mhe. Spika, swali jengine ambalo nataka kuliuliza ni kwamba kwa kuwa tunajua katika kila meli kuna idadi maalum ya abiria pamoja na kiwango maalum cha mizigo ambayo inapakiwa. Kwa utaratibu uliopo hivi sasa meli zetu zinachukua mizigo bila ya kujua ni tani ngapi mizigo ile, isipokuwa kuna suala la *approximation* tu, yaani labda wanakisia tu ni tani ngapi.

Kwa hivyo, ni lini hasa wizara hii itajidhatiti kupima mizigo kwa uhakika kama ni tani tatu au nne ama tano, yaani kama vile magari yanayopakiwa mizigo halafu ikapita ikajulikana gari hii imechukua kiwango gani ya mizigo. Sasa ni lini hasa tutapata chombo hicho cha kupimia mizigo.

Mhe. Spika, sasa niende kwenye ushauri. Kwa kweli ushauri wangu ambao nataka kuutoa kwa wale wafiwa au hamna ushauri. *(Makofi)*

Kwa kuwa fedha zipo za kutosha ambazo bado hazijajulikana utaratibu wake, basi napenda kumuuliza Mhe. Waziri kwamba fedha hizi zinaweza kutumika kwa ajili ya kumbukumbu ya kuwekewa misikiti, ambapo misikiti hii itakuwa ni kumbukumbu ya hao wafiwa. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Swali jengine je, kutokana na fedha hizi hiyo meli itakayoweza kununuliwa tunaweza kutia jina kwa ajili ya kuwawekea kumbukumbu zao wale wafiwa, ili iwe ni kumbukumbu ya meli yao, yaani jina hilo litoke kwa lengo la wale waliofariki dunia.

Ahsante Mhe. Spika, *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nami naomba uniruhusu nimuulize Mhe. Waziri maswali matatu yatuatayo:-

(a) Mhe. Spika, mara zote serikali imekuwa ikituambia kwamba kipaumbele watapewa wazalendo na tunazo taarifa kwamba Wazalendo wa Kampuni ya *Coastal Fast Ferries* na *Sea Gull* wameomba kuleta meli za kisasa za abiria na mizigo kwa kupatiwa *guarantee* na serikali, lakini zipo taarifa kwamba serikali imewakatalia.

Sasa kwa nini serikali imewakatalia wazalendo hawa na badala yake ikakimbilia nje kwa ajili ya kuwatafuta wafadhili?

(b) Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 3 Mhe. Waziri amezungumzia kuhusu uingiaji wa abiria pamoja na upakiaji wa mizigo na amejisifu kwamba pale panakuwa na Bandari, ZMA, *ZRB* na Usalama.
Kwa hivyo, nadhani kabla ya kupakia mizigo na abiria kwanza hutangulia zoezi la uuzaji wa tiketi na Baraza hili mara zote tumekuwa tukisema kuwa Wazanzibari wanauziwa tiketi za ulanguzi kiholela.

Kwa nini hadi leo wizara yake haijamudu na inashindwa na inakusudia kuwaachia wauzaji wa tiketi za magendo na kuaathiri Wazanzibari ambao ni wanyonge? *(Makofi)*

(c) Mhe. Spika, meli ambazo zinapakia abiria na mizigo Unguja na Pemba zimekuwa zikipakia abiria hao pamoja na watoto hata bila ya kuwaelimisha katika uvaaji wa *Live Jacket*.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri aniambie ni wakati gani abiria hupaswa afundishwe kuvaa *Live Jacket* au ni wakati ule meli inataka kuzama? *(Makofi)*

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, kwanza naomba kwamba Taarifa au Kauli ya Mhe. Waziri tusiichukulie kama zile kauli nyengine za kawaida. Kwa nini nasema hivyo Mhe. Spika, katika *hansard* ya tarehe 24 Julai, 2011, ambapo suala hili ndipo lilipojadiliwa mara ya mwanzo.

Sasa wakati Mhe. Waziri akifanya majumuisho Mhe. Spika ulitoa maelekezo yafuatayo:-

> "Mhe. Waziri labda nitoe maelekezo unajua maswali ambayo Waheshimiwa Wajumbe wamekuuliza, kimsingi ni maswali muhimu sana na wengi tuliomo ndani ni sehemu ya mashahidi wa hayo. Sasa nadhani ungeyapokea kwa jumla na ukayafanyiakazi kwa undani sana na baadaye utuletee ripoti nyengine". *(Makofi)*

Kwa hivyo, hii Mhe. Spika, ilikuwa ni ripoti kutokana na maelekezo yako, ndio nasema hii kidogo inatufanya maswali yetu yawe mengi na kwa undani, kwa sababu kama ilikuwa inafanya majumuisho ya yale ambayo wakati ule hayakukamilika.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba niulize maswali yafuatayo:-

Kwanza kwa sababu ya utangulizi wangu niliotoa Mhe. Spika, nilitegemea ripoti au Kauli ya leo ya Mhe. Waziri ingejibu kwa kina zile *concerns* au

maswali ambayo yalitolewa wakati ule. Sasa yako baadhi ambayo nimeyaona humu, lakini nashindwa kushawishika kwamba yanatimiza kile kigezo ulichotoa kuwa yawe majibu ambayo ni ya undani sana.

Kwa mfano, Mhe. Spika, naomba kujibiwa katika ripoti ya wakati ule kwenye kamati lilitolewa pendekezo la kuangalia Kanuni za Usalama, kwa maana ya *Safety Regulations* za mwaka 2009 na hasa juu ya lile sharti la kutaka ndani ya masaa ya 48 wakati inapotokezea hitilafu wale wanaohusika wawe wametoa taarifa katika mamlaka husika.

Kwa hivyo, kulitolewa pendekezo kwamba kanuni hii iangaliwe. Sasa katika majibu ya Mhe. Waziri kuna haya maelezo tu, kuwa kanuni hiyo inafanyiwa kazi, lakini *specific* alipolitaja sikulisikia kwamba Mhe. Waziri kauli yake anasema nini juu ya suala hili? Sasa naomba Mhe. Waziri atulijibu hilo.

Mhe. Spika, jengine katika hayo maelezo ya kamati wakati ule palitoka suala kuhusu kasi ya ukaguzi wa vyombo vya baharini pamoja na suala zima la upungufu wa maofisa wanaoweza kufanya hiyo kazi ya ukaguzi kwa maana ya *Safety Officers*.

Sasa hili pia katika maelezo ya Mhe. Waziri halimo na wala sijui limefanyiwakazi kiasi gani, muda wa miezi sita na zaidi tangu ilipotolewa kauli hii kwamba kuongeza hawa *Safety Officers* ambao watakuwa wanafanyakazi hiyo? Naomba Mhe. Waziri anijibu.

Mhe. Spika, palikuja suala kuhusu Sera au Sheria ya Uingizaji wa Vyombo hivi, kwenye maelezo yake Mhe. Waziri hili ameligusia akisema katika *paragraph* hiyo naomba kunukuu.

Ripoti ya Mhe. Waziri inaeleza hivi:-

> "Kuhusu suala la Kanuni na Udhibiti wa Meli Chakavu, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano inakamilisha Kanuni ya Sheria Nam. 3 ya mwaka 2009 ya Mamlaka ya Usafiri Baharini, ambayo itaweka pamoja na mambo mengine umri wa meli itakayoruhusiwa kuingizwa nchini".

Mhe.Spika, swali langu ni kwamba sheria hii kama inavyoonekana ni ya tangu mwaka 2009, kwa nini mpaka leo tunapata maelezo kwamba wizara inakamilisha. Kauli hizi zitakamilika lini Mhe. Spika na kama ni hivyo basi serikali ituambie haioni kama kuna haja ya kuzuia kutunga sheria nyengine mpaka kwanza tukamilishe Kanuni za sheria ambazo zilizopo zinazoshindwa kutekelezwa? *(Makofi)*

Swali langu jengine Mhe. Spika, lipo kwenye suala uokozi. Kwa kweli moja katika mambo yaliyoibuliwa wakati ule wa mjadala wa Kauli au Maswali kwa Mhe. Waziri lilikuwa ni suala zima la vyombo vyetu kiasi gani vinajitosheleza kwa kuwa na maboya ya kutosha ya kuogelea wakati wa uokozi ikibidi. Sasa hili katika maelezo ya leo tuliyoletewa na Mhe. Waziri halikuguswa kabisa.

Kwa hivyo, naomba kujua kwa kiasi gani wizara imelifanyiakazi suala hili hasa ya Ripoti ya Meli ya *MV. Spice Islander I* kuonesha kwamba hilo lilikuwa ni moja ya matatizo makubwa yaliyopelekea upotevu mkubwa wa maisha ya watu wengi kutokana na kutokuwepo na maboya ya kutosheleza?

Mhe. Spika, swali jengine linahusu taarifa kuhusiana na hali ya hewa. Katika kauli yake Mhe. Waziri leo ametueleza na naomba kunukuu.

Ripoti ya Mhe. Waziri inaeleza hivi:-

> "Kuhusu utoaji wa Taarifa za Mamlaka za Hali ya Hewa ni kwamba taarifa hutolewa kila siku na Shirika la Utangazaji Zanzibar kwa kupitia television na radio (*ZBC*). Hivyo, tunawashauri wenye vyombo pamoja na wananchi kwa jumla kufuatilia na kusikiliza taarifa hizo.
>
> Aidha mamlaka baada ya kupata taarifa za hali ya hewa huziwasilisha taarifa hizo kwa manahodha kabla ya kuanza safari zao".

Swali langu Mhe. Spika, kutokana na maelezo hayo ni kwamba nikitizama Mhe. Waziri alipokuwa akifanya majumuisho wakati ule alitaja kitu ambacho leo hakukitaja, sasa sijui hiki kimeachwa au vipi.

Mhe. Spika, naomba nireje katika *hansard* ya tarehe 24 Julai, 2011, kwenye ukurasa wa 18, Mhe. Waziri alizungumzia kwamba sisi tunapata taarifa zetu za hali ya hewa kutokana na Mkurugenzi wetu wa Hali ya Hewa ambaye yupo hapa Zanzibar. Lakini hivi sasa tunafanya utaratibu wa kuweka Tawi la Idara hii pale bandarini na hii imekuja baada ya kuona kwamba hakuna urahisi au wepesi wa Idara ya hii ya Hali ya Hewa kwa Shirika la Bandari na Mamlaka ya Usafiri Baharini katika masuala ya hali ya hewa baharini.

Kwa hivyo, hizi ni juhudi za wenzangu ambazo wameziona na sisi tumeziona mapema. Kutokana na hali hiyo tunaamini hivi sasa badala ya kujenga jengo moja la Ofisi za *Terminal*, basi tutajenga tena ofisi ndogo kwa ajili ya *Division* moja ya Idara ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Zanzibar, ili na sisi pale tuwe na taarifa za hali ya hewa wakati wote tunapozihitaji.

Mhe. Spika, swali langu ni kwamba je hatua hii imefikia wapi, kwa sababu leo katika Kauli ya Mhe. Waziri haikugusia kabisa katika maelezo haya. La mwisho Mhe. Spika, katika maelezo au kauli ya Waziri amezungumzia suala la idadi ya abiria. Pia ile nisimnukuu vibaya naomba niisome amesema.

> "Meli za abiria zinapaswa kuchukua abiria kwa mujibu wa idadi ya abiria iliyopangiwa. Hata hivyo kumekuwa na tatizo hasa kwa abiria wanaokwenda na kurudi Pemba, hatua zinachukuliwa kwa mashirikiano ya ZMA na wamiliki wa meli kupata ufumbuzi wa kudumu wa suala hili."

Maelezo haya Mhe. Spika, yanaonesha kwamba bado suala hili halijapatiwa ufumbuzi. Nilikuwa nataka kujua kwamba kuna uzito gani kwa wizara na kwa wasimamizi wa mamlaka mbali mbali zinazohusika katika kutilia nguvu utekelezaji wa suala hili. Sababu moja kubwa iliyotajwa katika ripoti ya MV. Spice Islanders ni kwamb wingi wa abiria waliopakiwa takriban mara nne ya uwezo uliokuwa umeruhusiwa ndio sababu moja kubwa ya ajali ile.

Maelezo haya ya Waziri inaonekana kama vile bado wizara inashindwa kulifanyia kazi. Kuna ugumu gani katika kulitekeleza suala hili Mhe. Spika, hasa ikizingatiwa ile orodha kubwa waliotutajia watu mbali mbali ambao wapo bandarini ambao jukumu lao ni kuhakikisha usalama wa vyombo hivi. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi na mimi nikulize masuali mawili matatu katika taarifa hii aliyoiwalisha Mhe. Waziri. Mimi nianze katika ukurasa wa 3, paragrafu ya pili kutoka juu, kuhusu kuahirishwa safari za mara kwa mara kwa vyombo vya baharini. Mimi nilikuwa nataka kujua maana yake imesemwa,

> "Kiutaratibu maana yake inasemwa haitakiwi kufanya hivyo ila kwa sababu maalum za msingi pindipo ikitokezea kuahirishwa kwa safari hizo bila ya sababu hiyo, vyombo hivyo hutozwa faini"

Nilikuwa nataka kujua ni vyombo vingapi ambavyo wameshavitoza faini na ni kiasi gani zilipatikana. Lakini baada ya kutoza faini vile vyombo wale abiria ambao wanapata usumbufu ni hatua gani ambayo wanachukua katika kuwasaidia wale abiria ambao wameahirishiwa zile safari pasi na sababu za msingi. Maana unafika pale Bandarini ndio unakuta safari imeahirishwa. Nilikuwa nataka kujua ni hatua gani wanazochukua kwa wale wenye vyombo juu ya hawa abiria ambao wanapata tabu kuahirisha safari zile.

Mhe. Spika, jengine katika ukurasa huo huo wa 3 katika suala la uingiaji wa abiria na upakuwaji wa mizigo, ameonesha hapa ingawa wenzangu waliuliza sana suala hilo na mimi nalirejea tena kwamba linahusu idadi ya abiria. Ukizingatia kwamba ule wingi wa maafisa ambao wanakuwa wapo pale. Nitaka kujua ni sababu zipi za msingi zinazopelekea meli zile zikawa zinaongeza idadi ya abiria wengi hata kuliko ule uwezo wa abiria wanaotakiwa kupanda katika meli ile.

Kwa mfano katika meli ya *MV. Spice Islander* tukisoma kwa mujibu wa hiyo taarifa iliyoletwa ile meli ina uweza wa kuchukua watu au abiria 610, lakini ilikuwa ina watu elfu mbili na zaidi. Sasa ukiangalia hapa mimi napata mshangao sana. Nataka hebu Mhe. Waziri atusaidie katika hili ni sababu zipi hasa zinazofanya wale wabiria wanakuwa mara tatu ya kile kiwango kinachotakiwa kupakiwa katika meli ile.

Mhe. Spika, jengine nateremka kwenye paragrafu nyengine sehemu ya Ukaguzi wa Vyombo vya Baharini, kwenye kufuata kanuni na taratibu zake. Nilikuwa nataka kujua hivi vyombo vyetu hapa vinakaguliwa katika utaratibu huo. Na sasa hivi tunavyo vyombo vingapi na vyote vimeshakaguliwa. Nilikuwa nataka kujua hilo.

Nirudie katika suala la muuliza mwanzo aliuliza Mhe. Abdalla juu ya ukaguzi wa chini . kweli hizi meli zetu zinakwenda kufanyiwa ukaguzi huo. Tunataka kujua hilo. Jengine kwenye paragrafu ya 6, nafikiria inasema kwamba, meli za abiria zinapaswa kuchukua abiria kwa mujibu wa idadi ya abiria iliyopangiwa.

> " Hata hivyo imekuwa kuna tatizo hasa kwa abiria wanakwenda na kurudi Pemba hatua zinachukuliwa kwa mashirikiano ya ZMA na wamiliki wa meli kupata ufumbu wa kudumu wa suala hili".

Hapa miye kidogo napata tatizo Mhe. Spika, meli za abiria zinapaswa kuchukua abiria kwa mujibu wa idadi ya abiria wanaotakiwa. Sasa anavyonambia kwamba kumekuwa na tatizo. Tatizo ni nini? Mpaka kukawa kunazidishwa hawa abiria. Maana yake anasema "tunataka tupate ufumbuzi wa pamoja baina ya wamiliki na *ZMA*" Kwa nini mna- *negotiate* wakati imeshapangiwa hii ni 310 kwa nini isichukue wale 310 mna- *negotiate* kuongeza au vipi. Nilikuwa nataka ufafanuzi katika hili, sikufahamu vizuri paragrafu hii Mhe. Spika.

Lakini vile vile nilikuwa nataka kujua serikali ina meli ngapi, ikiwa za abiria, ikiwa za mafuta, ikiwa za kubeba kokoto, ikiwa za kubeba lami nataka kujua serikali ina meli ngapi na ziko wapi na zinafanya kazi gani. Nataka kujua serikali ina meli ngapi? Lakini natakujua vile vile meli hizi je, zinaendeshwa

kwa faida. Na nilikuwa nataka mchanganuo kidogo kama itawezekana atupatie Mhe. Waziri kwa kila meli zinavyofanya kazi kwa mwezi mzima mapato yake na matumizi yake. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi kuuliza mswali katika ripoti hii. Na mimi nitaanza ukurasa wa 3 paragrafu ya kwanza ripoti imesema kwamba linapotokea suala la uokozi serikali hushajihisha vyombo vya baharini na angani kwa ajili ya uokozi.

Nilikuwa nataka kujua kwamba Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ina vyombo vya angani vya uokozi?

Suali hili litakwenda katika utaratibu wa safari za Unguja, Pemba na Dar-es-Salaam. Wizara ya Miundombinu kama muhusika mkuu inaweza kutuelezea kwamba.

Ni sababu zipi zinazopelekea kutofautiana kati ya nauli ya kutoka Dar kuja Zanzibar na kutoka Zanzibar kwenda Dar kwamba nauli ya kutoka Dar kuja Zanzibar iko chini lakini kutoka Zanzibar kwenda Dar iko juu. Ni sababu zipi zinapelekea kutofautiana kwa nauli hizi.

Serikali kupitia Wizara hii ya Miundombinu haioni kwamba ipo haja sasa ya kulichukulia hatua suala hili la kutofautiana kwa nauli ili kuwepo na *stability* ya nauli kati ya rudi hizi mbili, kwa sababu masafa ni yale yale na huduma ukiwa safarini ni zile zile. Ahsante.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza masuala ambayo yanojaa ukurasa sichini ya masuala 10 kwa kuweza kumuuliza Mhe. Waziri. Nitaanza na ukurasa wa pili hapa linalohusu suala la Wizara kuweza kutafuta fedha. Je, namuuliza Mhe. Waziri zile fedha zilizouzwa meli ya MV. Mapinduzi ziko wapi, hata serikali iweze kutafuta fedha nyengine?

Ukurasa wa 3 Mheshimiwa sasa hivi kuna tatizo kubwa kati ya vyombo hivi kwamba havina *time* ya kuondoka. Je, Mhe. Waziri hili unalionaje ili kuondosha lisije likatokezea tatizo la vyombo kugongana kwa kuwaondoka kwa pamoja.

Mheshimiwa kuhusu utaratibu wa kupakia idadi ya watu. Nakumbuka mimi katika hizi meli kuna kitu kinaitwa *booklet* kama nimekikosea basi naomba radhi. Sijui vyombo vyetu mabuku hayo yamo? Ambayo hayo yanaonesha idadi ya upakiaji wa mizigo na idadi ya upakiaji wa ajiria. Kama vyombo

ambavyo vinagundulikana havinavitu kama hivyo je, wizara yako inachukua hatua gani ili kuokoa wananchi wasiendelee kufa.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, napenda kumuuliza Mhe. Waziri, Katika hotuba yake Mhe. Rais alisema kwamba meli ya Kilimanjaro III itafanya safari ya kwenda Pemba. Lakini kwa bahati meli hii ni juzi tu ilikwenda Pemba kuchukua viongozi kuleta Unguja. Je, ni sababu gani ambazo meli hii haiyendi Pemba. Lakini vile vile meli ya Kilimanjaro II ilikuwa haiyendi Pemba kutokana na Mkondo kuwa mkali, lakini baadaye sasa hivi inakwenda Pemba. Je, ni sababu zipi ambazo zinapelekea kwenda Pemba na MV. Kilimanjaro III ikawa iyendi Pemba.

Mhe. Hassan Hamadi Omar: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii kumuuliza suala Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano. Kwanza kabisa suala langu nilitolee maelezo.

Nchi yetu ya Zanzibar ni Visiwa vilivyoungana Unguja na Pemba, lakini baada ya visiwa hivyo viwili kuna na visiwa vidogo vidogo vinavyoishi watu wengi kikiwamo Kojani, Fundo, Kisiwapanza, Makoongwe na visiwa vyenginevyo vidogo vidogo. Lakini nimeshtushwa na taarifa hii kuwa serikali kwa sasa hivi haina mpango wa kupata boti ndogo ndogo juu ya visiwa kama hivyo nilivyovitaja.

Mhe. Spika, ikumbukwe kwamba visiwa hivyo vinawatu, wanatoka ndani ya visiwa vyao na kwenda sehemu nyengine kwa mujibu wa shughuli zao za kikazi. Halafu ikumbukwe kunatokea ajali mbaya kama zinavyotokea ajali nyengine zinavyotokea Unguja na Pemba kwa mfano kama ajali iliyotokea kisiwani Kojani walipotoka watu wa Kangagani kwenda kuoa Kojani na ikazama vile vidau tunavyovukia na ikatokea ajali mbaya maharusi na wale wanalikwenda harusini wakazama baada ya harusi ukawa msiba. Ni lini serikali itakuwa na mpango wa kupata boti zenye usalama wa kusafiria visiwa kama hivyo kama ilivyokuwa hapo zamani.

Mhe. Spika: Sasa ni zamu ya majibu na kwa kuwa masuali mengine yamekwenda kwenye Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais kwenye suala la maafa basi nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais aanze kutoa majibu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi. Aidha niwashukuru Mhe. Waziri kwa kuwasilisha taarifa hii nzuri katika Baraza lako hili tukufu pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kwa masuala yao ambayo ni ya kutaka ufafanuzi ili kuelewa hali halisi.

Mhe. Spika, masuala ambayo yamegusa katika sekta yangu ni haya yafuatayo. Kwanza lilikuwa linahusu ni kiasi gani cha fedha zilizochangiwa kutokana na wahisani, wananchi na wafadhili mbali mbali kwa nia ya kuwasaidia waliokubwa na maafa ya ajali ya MV. Spice Islander I. Jumla la ya fedha ni bilioni moja. milioni mia mbili thalathini, laki mbili na elfu tatu, mia nane na sitini na moja, fedha hizo zote ziko katika Benki ya Watu wa Zanzibar katika *Account* maalum na kubwa tulikuwa tukisubiri ripoti ya Tume ili fedha hizo ziweze kugaiwa kwa wahusika.

Na sasa kwa kuwa ripoti ya tume tayari imetoa idadi ya waliokubwa na mkasa ule wa ajali ambao kwa jumla ni watu 2,473 hivi sasa tunayo ithibati inayotuwezesha mgao huo kufanyika. Kwa hivyo mara tu baada ya kufikia hatua za mwisho za maelekezo ya serikali, mgao huo utafanyika muda sio mrefu kuanzia sasa.

Mhe. Spika, madhumuni ya michango ile ni kusaidia wale waliohusika na ajali iliyotokea kwa maana ya waliofariki na walionusuruka ndio ambao zile ni fedha zao. Fedha zile hazikutolewa kwa ajili ya kununulia meli nyengine. Zile ni fedha za wahusika hao kutokana na maelezo ya waliozichangia.

Mhe. Spika, kuhusu ripoti kupewa waheshimiwa Wajumbe la Baraza la Wawakilishi. Hivi sasa ripoti ile tayari ipo kwenye Website na karibuni itawasilishwa pale Maktaba Kuu ya Serikali ili Waheshimiwa Wajumbe na wananchi wote wapate kuiyona. Lakini kwa sababu lile ripoti lenyewe ni kubwa sana, *booklet* nyingi sana.

Kwa hiyo itatubidi kutanye *summary* kama ambavyo alivyowasilisha Katibu Mkuu Kiongozi na Katiba wa Baraza la Mapinduzi, ili tuweze kuwagaiya wajumbe. Nachukua dhamana hiyo kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu tutahakikisha kwamba Waheshimiwa Wajumbe wanagaiwa ili *summary* ya ripoti kama ilivyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi.

Kuhusu vyombo vya Fedha ambavyo viliahidi vitasaidia watoto yatima wanaohitaji mabenki. Mhe. Spika, kazi yetu ni kuratibu nay ale maombi yote ambayo yataletwa yanayohusu watoto yatima wanaohitaji msaada huo kwa mabenki basi yale mabenki tunayo na mara tutakapopata maombi yale Wizara kwetu tutawasilisha kwa wahusika ili watoto hao waweze kusaidiwa. Hata hivyo serikali inaelewa tokewa mwaka 1964 imekuwa ikisaidia watoto yatima kupitia vifuo vyake vya kulelea watoto yatima.

Kuhusu hatua gani zilizochukuliwa na serikali. Mheshimiwa sote ni mashahidi tumeona kwamba zipo hatua za kisheria zimechukuliwa na hatua za kinidhamu

zimechukuliwa kwa wahusika na watendaji wengi wamesimamishwa kazi wakati wa hatua za kisheria zinachukuwa ili mkondo wa sheria upate nafasi yake.

Kuhusu suala la fidia. Mhe. Spika, fidia inalipwa na Bima kwa mujibu wa Sheria Nam. 5 ya mwaka 2006 ya Usafiri wa baharini. Kama kwamba sheria ile ilieleza vizuri kunakuwa na uzembe ima wa Mwenyekumiliki mali hiyo kwa maana ya chombo hicho au wafanyakazi wake ama wakala wake, basi kifungu 394 cha sheria hile inamtaka fidia hiyo alipe mwenye kumiliki chombo hicho.

Kwa hiyo Mhe. Spika, hayo hasa ndio mambo ambayo yanihusu kwa upande wangu. Naomba kutoa taarifa hiyo. Nakushukuru naomba kuwasilisha Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku hii ya leo kuwa njema kwetu.

Aidha niungane na wewe kumshukuru sana Mhe. Waziri katika uwasilishaji wa ripoti hii. Napenda kuchukua nafasi hii kujaribu kujibu baadhi ya masuala ambayo yameulizwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Spika, kwa kuanzia nitaanza na hoja za Mhe. Hassan Omar aliyeuliza au aliyetaka kujua ni lini serikali itanunua meli ndogo ndo au mweli ndogo ndogo kwa ajili ya visiwa vidogo vidogo.

Mhe. Spika, ni dhahiri kwamba kwa kipindi hichi kiu na azma ya serikali ni kununua meli kubwa itakayoweza kutoa huduma za usafiri kwa maeneo ya Unguja /Pemba, Unguja /Dar-es-Salaam, Pemba /Tanga na hivyo kwa kipindi hiki serikali tutaendelea kurejea kauli yetu kwamba hatuna mpango wa kununua boti ndogo ndogo kwa ajili ya usafiri wa ndani. Lakini tutatumia nafasi hii kuwashajihisha wafanyabiashara wetu na wawekezaji kuweza kutumia fursa hiyo kwa ajili ya kufanya biashara na kupata kipato zaidi kwa shughuli zao hizo za kibiashara.

Mhe. Spika, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi alitaka kujua ni sagani zilizopelekea MV. Kilimanjaro III kushindwa kwenda Pemba na Boti ya Kilimanjaro II ambayo hapo kabla ilikuwa ikizuia safari za kwenda Pemba na hivi sasa kuruhusu safari za kwenda Pemba.

Mhe. Spika, hivi ni vyombo vya mtu binafsi, bila shaka yeye anaangalia maslahi yake kifaida. Lakini pia pengine inawezekana kukawa na upungufu wa vyombo kwa ruti ya Dar-es-Salaam na Zanzibar ndiyo iliyopelekea. Tunaamini

kama wito alioutoa Mhe. Rais wakumuomba mmiliki huyu kuruhusu vyombo vyake hasa hichi cha MV. Kilimanjaro III kwenda Pemba. Tunaamini atazingatia ombi hilo la Mhe. Rais na yeye atatekeleza kwa vitendo, baada ya kuanza na utaratibu wa meli hii ya MV. Kilimanjaro II.

Mhe. Spika, nije kwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ametaka kujua fedha za meli iliyouzwa MV. Mapinduzi ziko wapi. Mhe. Spika, ni kweli serikali ilifanya maamuzi ya kuuza meli ya MV. Mapinduzi kwa mfumo wa fedha *out* na fedha hizo zipo, zipo Hazina, lakini fedha hizo hazikidhi kununua meli mpya. Fedha hizo zipo salama katika mikono ya serikali.

Mhe. Spika, pia alitaka kujua ratiba za meli. Miongoni mwa mambo ambayo yanatusumbua ni kukosekana kwa kanuni. Kanuni zinazoweza kutupa sisi mamlaka ya ZMA kupata nguvu ya kusimamia katika upangaji wa ratiba. Hichi ndicho kinachopelekea baadhi ya vyombo kushindwa kuheshimimu maelekezo wanayopewa.
Lakini tunaamini kwamba tutakapoweza kukamilisha kanuni hizi tutakuwa tuna nguvu za kisheria zitakazowalazimisha wamiliki wa vyombo hivi kufuata utaratibu na maelekezo tunayowapa katika utaratibu wa kufuata ratiba.

Mhe. Spika, pia alitaka kujua utaratibu wa kupakia abiria. Mhe. Spika, utaratibu unatumika wa kupakia abiria na mizigo katika vyombo vya baharini ni kwa kuzingatia kitabu kinachoitwa *stability booklet* ambayo ndiyo inayotoa uwezo wa chombo husika katika kuhimili mzigo kwa kiasi gani kinastahiki kupakiwa na si vyenginevyo.

Mhe. Spika, Mhe. Wanu Hafidh Ameir alitaka kujua suala la uwokozi kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inavyo vyombo vya angani kwa uokozi au laa. Mhe. Spika, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia vyombo vyetu vya ulinzi na usalama inapotokea dharura huwa tunashirikiana nao kupata vyombo hivyo vya uokozi ikiwemo erkopta na vyombo vyengine.

Aidha wawekezaji wetu waliokuwepo nchini wapo wanaomiliki erkopta nao hushirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya uokozi na ndivyo ilivyokuwa katika tukio hili la MV. Spice Islander lilipotokea.

Mhe. Spika, pia Mhe. Wanu alitaka kujua ni sababu zipo zinazopelekea nauli ya kutoka Dar-es-Salaam kutofautiana na ile ya Zanzibar. Mhe. Spika, hili tumelichukua na sisi tutalisimamia katika kuona utekelezaji wake. Lakini uwezo wetu sisi ni kusimamia nauli ya kutoka Zanzibar kwenda Dar-es-Salaam na tutaomba wenzetu wa *SUMATRA* watusimamie upande wa kutoka Dar-es-

Salaam kuja huku ili kuonesha ushabihiyano wa taasisi hizi mbili katika ufanyaji kazi kutoa huduma kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, Mhe. Mbarouk Mussa (Mtando) alitaka kujua ni vyombo vingapi ambavyo vimetozwa fain. Kama taarifa ya Mhe. Waziri inavyoeleza kwamba kiutaratibu chombo hakitakiwi kurudi na inapotokezea kurudi basi kiwe kinarudi kwa dharura. Na hiyo ndiyo hali halisi ilivyotokezea. Mpaka muda huu Mhe. Spika, hakijatokezea chombo ambacho kimerudi au kukatisha safari pasi na saabu za msingi. Kwa msingi huo hakuna chombo ambacho tumekipiga faini kwa kufanya hivyo. Kwani hakuna ambaye amefanya kosa hilo, kama sheria zinavyotuhitaji.

Mhe. Spika, nadhani itakuwa pia tumejibu hoja alizotaka kujua ni hatua gani za ziada zilizochukuliwa kwa chombo ambacho kimekatisha safari. Majibu yetu ni kwamba hakuna chombo ambacho kimekatisha safari kinyume na utaratibu.

Mhe. Spika, pia Mhe. Ismail Jussa alitaka kujua kwa undani suala la maboya ya abiria yalifanyiwa kazi kwa kiasi gani. Utaratibu ni kwamba kila chombo kinatakiwa kuwa na idadi ambayo itaendana na uhalisia wa idadi ya abiria, kwa mfano kama meli itakuwa inachukua watu 500 tumewataka kuwahimiza kwamba life jaket zao ni lazima zikidhi ile idadi ya watu 500 na kupindukia na sio kuwa na idadi chini ya idadi ya abiria ambayo imeruhusiwa kuchukua.

Mhe. Spika, kuhusi na suala la taarifa ya hali ya hewa. Napenda kuungana nae Mhe. Mwakilishi bado katika suala la ujenzi wa Afisi katika eneo letu la Bandari hatujalitekeleza. Lakini katika hili tumejaribu kutanua wigo kwa kurahisisha mahusiano zaidi na taasisi yetu hii ya utabiri wa hali ya hewa. Na imekuwa kawaida kila siku asubuhi tunapashana taarifa kwa maandishi katika kufanikisha kuona kwamba taasisi hizi mbili zinashirikiana katika kufanya kazi kwa karibu ili kuweza kuwasaidia wananchi katika kupata taarifa sahihi za utabiri wa hali ya hewa. Kunusuru vyombo pamoja na wasafiri wao.

Mhe. Spika, pia Mhe. Jussa alitaka kujua suala la upakizi wa abiria ugumu wake uko wapi. Napenda tena kurejea kauli ya Mhe. Waziri kwamba utaratibu huu kweli tumejidhatiti kufanya hivyo kuzuia suala la abiria. Lakini tumekuwa tukipata changamoto inayotokana na wasafiri hasa wanaokwenda Pemba. Changamoto hii inachangiwa na mapungufu ya Kanuni yanayotukwanza sisi katika kutambua, nani ni abiria halisi kwa mujibu wa umri wake. Tumekuwa tuna changamoto kubwa hasa ya vijana ambao wapo chini ya umri wa miaka 12, tumeshindwa kuwadhibiti kwa kujua idadi gani wanastahiki kupanda katika chombo ikiwa wanaambatana na na wazazi wao.

Imani yetu kwamba baada ya kukamilisha kanuni hizi zitaweze kutuelekeza na kutupa msaada mzuri wa kuweza kutambua umri gani ambao unastahiki kumuhesabu kama abiria na kumri gani ambao haustahiki umuhesabu kama abiria. Mategemeo yetu kwamba tukiweza kuziimarisha kanuni zetu hizi tutaweza kupata umbuzi katika tatizo hii la kuongeza abira hasa watoto wadogo.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija alitaka kujua ni kikwa gari kilichotufanya sisi serikali kushindwa kuweka dhamana kwa wawekezaji wa ndani ikiwa kampuni ya *MV. SeaGull* na Kampuni ya *COSTAL FERRIES*. Mhe. Spika, haya ni Makampuni binafsi, serikali haina kipingamizi kwao na naamini kama wana nia kama walivyoweza kufanya hizo biashara nyengine na kwenye hili serikali itawapa ushirikiano.

Mhe. Spika, pia alitaka kujua uuzaji wa tiket kiholela, alitaka kujua kikwazo ni nini. Mhe. Spika, hapa naomba nitoe wito kwamba sisi wizara tunachokifanya sisi ni kusimamia na kupanga na wenzetu. Mfano tiket tuuze Sh. 20,000/-, jambo la kusikitisha ni kwamba abiria anakwenda kidirishani tiketi imeandikwa Sh. 20,000/= lakini yeye anahimili kulipa kwa Sh. 40,000. Unapomtaka yeye akupe ushirikiana wa kutambua aliyefanya uhalifu ule yeye anakuwa hayupo tayari kufanya hivyo. Sisi kama Wizara tutaendelea kufanya nao kazi wenzetu hawa wanaouza tiket au wamiliki wa vyombo kwa kuomba kwamba wasimamie yale maelekezo tunaowapa. Lakini pia tunaiyomba jamii na wao pia wawe tayari kushirikiana na mamlaka husika katika kuwatambua hawa wahalifu ili kuweza kuondoa usumbufu huu wanaoupata wananchi wetu.

Mhe. Spika, pia Mhe. Hija alitaka kujua ni muda gani ambao abiria anapaswa kuelekeza namna ya kuvaa jaket la uokozi. Mhe. Spika, kama ulivyo utaratibu mwengine abiria anatakiwa kupewa maelekezo na mafunzo ya kuvaa jaketi hili la uokozi kabla ya safari kuanza. Matarajio yetu kwamba wamiliki na mabaharia wa vyombo husika vya abiria wanatekeleza maelekezo hayo kwa vitendo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Suleiman Khamis alitaka kujua fedha gani zimepatikana nadhani Mhe. Waziri wa Nchi ameshalitolea ufafanuzi. Suala la Serikali itapata lini meli mpya tayari pia limetatolewa ufafanuzi lakini maelezo zaidi atayaleta Mhe. Waziri.

Na utaratibu wa upakiaji wa mizigo kama tulivyoeleza kwamba utaratibu wetu sisi tunafata *stability booklet* ambacho ndio chombo kinacho regulate kuonesha uwezo halisi wa chombo husika katika upakizi wa mizio, ndicho chombo tunachokifata.

Mhe. Hamza alitaka kujua suala la uzimamizi wa kiwizara zimechukuliwa hatua gani. Mhe. Waziri atakuja na majibu kwenye hilo.

Mhe. Saleh Juma alitaka kujua serikali ina mpango gani kuhusiana na utaratibu gani kutoka Pemba kwenda Tanga. Kama tulivyoeleza kwamba nguvu zetu tumeelekeza kupata vyombo vikubwa kitakachoweza kutoa huduma Unguja/ Pemba, Unguja/Dar-es-salaam. Pemba/Tanga na maeneo mengine, lakini sio ku tafuta vyombo vidogo. Nguvu zetu za serkali tunaelekeza katika kutafuta chombo kikubwa kitakachoweza kutoa huduma kubwa sana kwa wananchi wetu.

Aidha alitaka kujua suala la fedha za maafa . Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ameshalitolea ufafanuzi

Mhe. Spika, Mhe. Omar Ali Shehe aliuliza suala la ulanguzi wa tiket nalo pia tumeshalitoa ufafanuzi. Vile vile Mhe. Omar alitaka kujua Shirika la Meli tatizo walilolipata kushindwa kukamilisha katika zabuni ya upatikanaji wa meli kwa kampuni ile kutoka South Africa. Mhe. Spika, serikali iliona kwamba zabuni ile ni gharama kubwa na isingekuwa busara maana serikali ilizuia zabuni ile katika kufanikisha upatikanaji wa meli kwa kuona kwamba gharama zake ni kubwa iliiruhusu wizara yetu na Wizara ya Fedha kuendelea kufanya mchakato ili baadae kurejesha tena pendekezo serikalini. Lakini maelezo ya ziada Mhe. Waziri ataogelea katika eneo hilo.

Mhe. Spika, pia Mhe. Abdalla Juma Abdalla alitaka kujua utaratibu unaotumika katika ukaguzi wa meli hasa kwa kuzingatia na meli ya MV. Serengeti mara ya mwisho imefanyiwa ukaguzi lini na ripoti inasemaje. Mhe. Spika, kwenye hili Meli ya Serengeti inafanyiwa ukaguzi vielelezo vipo na ninaamini pengine hata akitaka *copy* za maandishi tunaweza kumpatia.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Bakari Makame alitaka kujua kwa kiasi gani wizara au serikali inaweza kumshawishi mwekezaji mwenzetu Bwana Bakhresa katika uwekezaji wa vyombo hivi. Mhe. Spika, sisi kama serikali tunajitahidi kutoa wito kwa wawekezaji wawe wa ndani au wa nje katika kuekeza katika eneo hili ni imani yetu kwamba Bwana Bakhresa wito huo ameusikia na sisi kama serikali hatuna pingamizi tutaendelea kushirikiana naye kama ambavyo tumekuwa tukishirikiana katika biashara kwa kuwa na meli nyingi zinazofanya biashara kati ya Zanzibar na Dar es Salaam. Tunaamini kwamba boti yake moja iliyoanza safari ya kwenda Pemba ataimarisha kutafuta chombo chengine kikubwa zaidi ili kuimarisha huduma hizi kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache nasema nakushukuru na namuomba Mhe. Waziri aweze kuyatolea ufafanuzi vizuri.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi nyengine ya kujibu maswali na hata kutoa ufafanuzi kwa yale mambo ambayo si maswali lakini yanaoneka ni maswali. Kwanza kabisa Mhe. Spika, nataka niwatambue wote ambao wamechangia au wameuliza maswali katika taarifa hii. Kwanza Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi ya Baraza lako tukufu, lakini vile vile wajumbe wengine 13 ambao Mhe. Naibu Waziri amekuwa akiwataja lakini kwa sababu ya muda naomba kama vile ambavyo wametajwa basi na mimi itakuwa nimewataja.

Mhe. Spika, kwanza nimshukuru kabisa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili kwa ufafanuzi wake kwa yale maswali ambayo yaligusa moja kwa moja serikali kuu. Lakini nimshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano japo amejibu kwa haraka haraka lakini naamini maswali yenyewe na majibu yenyewe yamefahamika. Kwa kweli mimi kazi yangu ni ndogo na naomba niende moja kwa moja.

Mhe. Spika, Mhe. Abdalla Juma Abdalla imeelezwa vizuri hapa na Naibu Waziri wangu lakini alitaka kujua ni lini hasa mara ya mwisho MV. Serengeti ilifanyiwa ukaguzi. Mhe. Spika, ni kwamba tarehe sina lakini utakumbuka kwamba MV. Serengeti ilipata ajali ya kuungua ikakaa kipindi kirefu sana katika matengenezo na mpaka iliporudi na matengenezo yale yalikuwa makubwa, baada ya matengenezo ya hapa ilikwenda *dry dock*. Kwa hivyo, tangu iliporudi *dry dock* na kuanza kazi haijafika miezi 18, hivyo tarehe rasmi ambayo imeenda *dry dock* nitamletea kwa sababu hapa sina.

Mhe. Spika, Mhe. Asha Bakari Makame ametoa pongezi kwa serikali pamoja na wajumbe wengine. Kwa hivyo, mimi nichukue fursa hii kuwashukuru vile vile kwa kutambua kwamba serikali imefanya juhudi yake kama serikali imeunda tume, tume ambayo ilikuwa na malalamiko lakini matokeo yake yamezima malalamiko yote. Mhe. Spika, bila shaka chochote utakachokifanya hata kiwe kizuri vipi kutakuwa na wengine wanakubali na wengine wanakataa na kila mtu ana mawazo yake. Lakini kwa ujumla ripoti ya serikali imepokelewa kwa sababu ni mara ya kwanza wanavyosema wengi kwa jambo kama hili au linalofanana na hili kutokea na serikali ikachukua hatua kama hizi ambazo zimechukuliwa. Kwa hivyo, nachukua pongezi hizo na nasema ahsante sana.

Mhe. Spika, jengine ambalo Mhe. Asha Bakari amelitaja ni kuhusu serikali kuwatumia wazalendo. Mhe. Naibu Waziri ameligusia hili lakini mimi nataka nitoe kauli hapa kwamba serikali inakaribisha wawekezaji wa namna zote na zaidi katika usafiri wa baharini, kwa sababu ndilo tatizo ambalo sasa hivi ni ajenda kubwa. Mhe. Spika, ni kwamba hakuna hata mmoja aliyeleta meli hapa ikakatiliwa, hakuna hata mmoja aliyetaka kuleta meli akaambiwa asilete.

Lakini kuna taratibu zake lazima zifuatwe huwezi tu ukasema naleta meli au ukachukua meli yako huko ikafika hapa ukasema mimi nimeshaleta meli halafu serikali ikasema haya. Kwa hivyo, kuna taratibu maalum na kuna sheria zake, lakini hakuna aliyetaka kuleta meli akakataliwa na kama yuko basi aseme mimi nilitaka kuleta kwa ushahidi huu na nimekataliwa kwa ushahidi huu. Mhe. Spika, sio hilo tu ni kwamba katika uwekezaji wa usafiri baharini, vyombo vya baharini ni ghali sana na sio kama ghali tu lakini hata kwa sababu ni *machine* hivyo wawekezaji wengi katika vyombo vya baharini wanakuwa na hadhari kubwa.

Mhe. Spika, serikali katika utaratibu wake huwa hainunui vyombo vichakavu au ambavyo vimetumika na hapa nataka nichukue nafasi kujibu swali la Mhe. Omar Ali Shehe na wengine. Kwa nini tumekataa kuchukua meli ambayo mikopo ilikuwa nafuu, serikali ni kudhamini tu au vyovyote vile. Mhe. Spika, ni kwamba serikali si kudhamini tu, serikali kama ni mkopo basi ule mkopo unaolipa ni serikali na kwa njia nyengine unayelipa ni wewe kwa sababu ni kodi ya serikali.

Mhe. Spika, meli ambayo ilikuwa inunuliwe ilikuwa iundwe Afrika ya Kusini kwa gharama ya dola milioni 25. Serikali ikasema kwa sasa hivi nguvu hii hatuna hata kama ni mkopo lakini huo mkopo vile vile nao unajiangalia naweza kulipa hii na kwa muda gani, na kwa sharti gani. Mhe. Spika, hiyo ilikuwa ni meli moja nataka nikupeni *breaking news.* Mhe. Spika, katika huu mchakato *process* ya kutafuta meli ambayo nimeeleza hapa serikali imeagiza wizara mbili kutafuta meli, na namna ya kupata meli hizo. Tumepeleka *specification* na masharti yetu tunataka meli ya namna hii, abiria wangi na iwe vipi.

Mhe. Spika, katika majibu tuliyopata kwa kampuni mbili, moja ya Kituruki na moja ya China hawa wametuletea bahati mbaya sikuzileta, lakini meli 3. Meli moja ya abiria 1000 na mizigo tani zaidi ya 400, meli nyengine ya mizigo tu na meli nyengine ya mafuta hizo ni meli 3. Mhe. Spika, kwa mujibu wa *specification* zetu zote hizo hazikufika dola milioni 35, zote 3 ni dola milioni 31, meli ya abiria 1000 haikuzidi dola milioni 13. Kwa hivyo, serikali kusema hili jamani hatuliwezi hii ni *proof* kwamba kumbe dola milioni 25 tungekuwa nazo tungeweza kununua meli nyengine hata 2, na wamesema watajenga meli hiyo kwa muda wa miezi 10.

Mhe. Spika, meli inachukua muda mrefu kujengwa kwa sababu meli inajengwa vile unavyotaka wewe ijengwe, kwa serikali haiendi tu meli zimepangwa kama gari ukasema nataka meli hii. Meli zinajengwa kutokana na mambo ambayo bandari zile meli itafanyia kazi, ukitaka kuleta meli Zanzibar lazima uwe mjenzi na si hilo tu mtu aje mwenyewe kuangalia, bandari ya Pemba, bandari ya Tanga, bandari ya Dar es Salaam na bandari ya Unguja, maana yake ndio

meli tunataka meli hiyo ifanye kazi humo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, suala la serikali kukataa mkopo wa dola milioni 25 kwa meli ya abiria mimi nauafiki kabisa na hili ni *proof* kwamba kumbe subira inavuta kheri.

Mhe. Spika, wizara mbili zimeagizwa na kazi zinafanywa specification tunazo na bado nyengine tunazingoja maana yake tunapeleka kama kwenye kampuni 8, walioleta *returning* ni kampuni 2 tu. Kwa hivyo, tunasubiri bado kwani kuna Korea, kuna Afrika ya Kusini na wengine pia walete lakini wakati tushajua angalau *basic* serikali inaangalia ni wapi tunapata mkopo nafuu ili tuingie katika mkopo huo serikali ipate ama meli moja au mbili au hata ikiwezekana meli tatu. Kwa hivyo, hili nimelifafanua makusudi ili Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu waone kwamba kuna juhudi zinachukuliwa.

Mhe. Spika, kuhusu Mhe. Hamza Hassan Juma mambo mengi yameshajibiwa, yale ambayo Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais mimi siyagusi ilikuwa ni kuhusu ripoti. Lakini lile ambalo linanihusu mimi nasema kwamba ripoti ile iliagiza mambo mengi, kuna hatua za kuchukuliwa za kisheria na za kinidhamu na hatua zote hizo kwa mujibu wa ripoti ile zimeanza kuchukuliwa. Kwa hivyo, haya mambo mengine yote mimi nasema hayo ni maamuzi ya serikali bado, na kwa sababu ni serikali basi naiachia serikali.

Mhe. Spika, lakini kubwa zaidi ni kwamba serikali imeanza kutekeleza na imeelezwa hapa kwamba tayari Rais ameshatengua uteuzi wa Wakurugenzi Wakuu wawili wa Mamlaka ya Usafiri Baharini na Shirika la Bandari la Zanzibar. Mhe. Spika, kuhusu Maofisa wengine inategemea walipatikana vipi, Mrajisi hatua zinachukuliwa, Mkaguzi wa Meli hatua zinachukuliwa na kwa sababu wameshtakiwa kama ambavyo ripoti imeagiza watavuliwa vyeo, watasimamishwa kazi kama ambavyo ripoti imeeleza. Kwa hivyo, hiyo kumuachisha kazi hizo nasema ni *displinary action* na serikali ina amini kabisa kwamba haitabakisha mtu katika ripoti ya tume.

Mhe. Spika, jengine ni kwamba hizi *legal action* nazo zinaweza kuchukuliwa kama mmesikia watu wameanza kukamatwa wamepelekwa polisi wamehojiwa na wengine wameanza kupelekwa Mahakamani. Mimi nasema ripoti hii inaiweka serikali pale ambapo serikali ilitaka kuwekwa.

Mhe. Spika, katika hili hadi sasa imechukua hatua gani nimeshasema. Je, meli ya *Spice Islander* ilifuata utaratibu wa kanuni za *MO*, je, hatua gani wizara itachukuliwa na serikali baada ya wizara hii kudharau maoni ya Wajumbe wa Baraza.

Mhe. Spika, hapa nataka nitofautiane sana na Mhe. Hamza, ni kwamba serikali wala wizara haijadharau unapomdharau mtu maana yake ni humuheshimu.

Maoni yote yaliyotolewa hapa yanachukuliwa na yanafanyiwa kazi, lakini si jambo la kufumba na kufumbua ukiniambia kwamba tunachukua mawazo yenu kuhusu utungwaji wa kanuni. Mhe. Spika, wewe ni mwanasheria na baadhi yetu hapa ni wanasheria na Mwanasheria Mkuu yupo, Waziri wa Katiba pia yumo kwamba kuna sheria zimetungwa huu ni mwaka wa sita na kanuni bado hazijesha kutungwa.

Mhe. Spika, sheria ya *ZMA* ilitungwa mwaka 2009 huu ni mwaka wa tatu baadhi ya kanuni zimetungwa na tunaendelea kutunga kanuni. Kwa hivyo, si jambo la siku moja au mbili au tatu mimi nasema wanasheria wapo, na kuna sheria hapa zimetungwa hadi hii leo sisemi kwamba mwenzako akiiba kwa hivyo na wewe uibe, lakini nasema suala la kutunga kanuni *is a process* na tunalifanyia kazi. Pia sasa hivi tunashirikiana na *SUMATRA* kuona kanuni zao zikoje ili na hizo tuzigeuze katika vifungu maalum kuanza kwetu, kwa sababu kuna mazingira mengine hatufanani na tumeunda kamati maalum ambayo ina wajumbe kutoka *SUMATRA* na *ZMA* kwa ajili ya kutunga kanuni hizi na tumewapa muda ili watupe *draft* ya hizo kanuni tukishakubaliana tutazipeleka kwa Mwanasheria Mkuu na yeye aziangalie. Kwa hivyo, hii ni *process* Mhe. Spika.

Mhe. Spika, Mhe. Suleiman Hemed ameeleza vizuri kuhusu fidia imeelezwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kuhusu hali ya hewa Mhe. Naibu Waziri wangu ameeleza vizuri, lakini niongeze zaidi ni kwamba watu wa *TMA* tulikubaliana kwamba waweke kituo pale lakini kwa taarifa yetu ni kwamba pale ambapo tulitakiwa wao wapate kituo. Ni kwamba kuna mradi wa *passenger terminal* ambao sasa hivi watu watakaoekeza akiwemo mzalendo, Bwana Bakhresa wakishirikiana na *Zanzibar Social Security Fund* wanataka kuekeza katika *terminal building* kiasi cha zaidi ya dola milioni 15 ambapo mahali pote pale sasa hivi patabadilika kabisa na hatua ziko mwishoni. Kwa hivyo, tungesema tujenge pale ili *TMA* waje wachukue wakati kumbe si muda mrefu pale pahali patabomolewa.

Kwa hivyo, tumekubaliana kwamba bado waendelee kuteletea taarifa hizi kwa sababu isingekuwa vizuri kuweka kituo pale sasa hivi wakati kituo hicho kesho na keshokutwa kitavunjwa. Kwa hivyo, wangejenga sio kwa gharama zetu wangejengwa kwa gharama zao na ile ni Serikali ya Muungano na sidhani kama Serikali ya Muungano wako tayari kuja kuwekeza pale halafu baada ya muda wakaambiwa hapa muondoke, ni kwamba sisi tulikuwa hatujui. Kwa hivyo, tumewaarifu hilo lakini bado dhamira yetu ni kuwa tuwe na tawi la TMA kwa ajili ya urahisi wa hizi taarifa. Mhe. Spika, hilo sikuligusa kwenye taarifa yangu lakini maelezo yake ni hayo niliyoyatoa.

Mhe. Spika, ni lini Shirika la Bandari litapima mizigo kwa uhakika? Mhe. Spika, mizigo katika meli ni tofauti na mizigo katika ndege. Katika ndege kuna vipimo na mizigo wenyewe sio mikubwa, lakini katika meli ukisikia meli ya mizigo maana yake ni kwamba ile mizigo wenyewe inajuulikana, mtu anakwambia nina tani zangu 25 za unga, watu wanapakia wanajua kwamba polo moja la unga ni kilo 50.

Kwa hivyo, tani 25 ni polo ngapi wanafanya mahesabu zinawekwa hapo zinapakiwa. Kwa hivyo, hivyo ndivyo kwa urahisi tunavyoweza kupima mizigo inayoingia katika meli, mizigo hii ya mkononi aliyekuwa na mkoba wa ukili, aliyekuwa na ndizi mkononi hii mizigo ni kwamba utaratibu wa abiria ni kuwa anachukuliwa akiwa na mizigo yake.

Mhe. Spika, ndio maana wakizidi zaidi ya hapo basi ndio haiendi lakini sio kama mnaingia mle mnapimwa. Kwa hivyo, utaratibu huu wa mizigo katika meli ndio ulivyo kwa mizigo mikubwa na mizigo midogo huwa haipimwi abiria anapewa asilimia 30 ya uzito wake kwamba atakuwa na mzigo. Kwa hivyo, hiyo ndio inachukuliwa kwamba ndio *tonnage* ya hiyo meli wenyewe. Kwa hivyo, kwa kifupi ni kwamba mizigo inapimwa lakini kwa utaratibu huu ambao nimeueleza hapa, si ule utaratibu wa kwenda na mizani pale halafu ukaanza kupima.

Mhe. Spika, Mhe. Hija Hassan Hija hakuna mzalendo yoyote wala sio mzalendo tu hata mtu wa kigeni aliyetaka kuleta meli hapa akakataliwa. Lakini ninachosema ni kwamba huko nje kuna mambo mengi yanazungumzwa, Mhe. Spika, kuna mzalendo ana kawaida ya kuleta meli ameshaleta meli tatu hapa. Na meli nyengine ya nne aliyotaka kuleta amekwenda huko na watu wake imeletwa *interim certificate* kwamba amesharuhusiwa na hao ambao amekwenda kununua hao wauzaji, kwa sababu lazima upeleke *return* kuna meli hii tunaileta huku mnaikubali.

Mhe. Spika, tulipoangalia ni kwamba amechukua *certificate* ya meli alizokwishakuleta akabadilisha jina lakini *all other particulars* ni za meli hii ambayo ameshaleta inafanya kazi. Mhe. Spika, ameleta taarifa hiyo ikiwa serikali imesharuhusu yeye kuleta hiyo meli, hii ni *forgery* tena kubwa na serikali haiwezi kukubali tukasema hapana, hii ni *forgery* sisi *certificate* hii hatuna rikodi yake. Mhe. Spika, tulipoangalia kumbe amefuta jina ya meli moja alizoleta akaweka jina lile pale.

Mhe. Spika, hakuna ufundi kama kusema uongo, ili useme uongo uwe fundi kweli kweli na uwe husahau. Wewe leo ukiulizwa na mtu asiyekujua jina lako nani ukisema naitwa Bakari, kumbe ni Pandu Ameir Kificho anaweza akaja akauliza Bakari yuko wapi hapa, na upo na anakuona ukanyamaza kimya,

lakini angesema Pandu Ameir Kificho ndio mimi. Kwa hivyo, lazima unaposema uongo ujue kwamba hakuna ufundi kama kusema uongo, uwe fundi kweli kweli ndio useme uongo.

Mhe. Spika, kwa hivyo watu wa namna hii hatuwezi kuwaruhusu kuleta meli na kama hii ndio labda ilichukuliwa kwamba tumekataa, ni kwamba tumekataa kweli kwani hatuwezi kukubali *forgery* akaleta pengine meli mbovu hapa halafu akasema serikali imeniruhusu na leo hii hawataki kuniruhusu kufanya safari, maana yake ndio mwisho yanakuja hayo. Mhe. Spika, mtu anasema wameniruhusu na *certificate* hii hapa na meli ameshaileta hapa na amelipa tena kwa mkopo, ni kwamba wamechukua mkopo benki halafu amezikwambisha huko, halafu kitu kama hicho cha thamani kubwa unafanya *forgery*. Mhe. Spika, tuko makini sana kwa hilo.

Mhe. Spika, katika usafiri wa baharini kuna mambo mengi na wenzetu wanapeleka huko ni vizuri sisi tuwapate vile vile. Mtu anakaguliwa mara tatu anaambiwa hapana anasema yeye sikubali anataka mkaguzi mwengine, tunamwambia mlete basi anamleta kwa gharama zake na tushirikiana naye mkaguzi wake mwenyewe basi anasema hii meli haifai isende. Halafu anasema kwamba mmeleta mkaguzi wangu kasema meli iende lakini serikali hawataki, sisi tunajua jamani tatizo la usafiri hasa Unguja na Pemba ni kubwa, lakini pamoja na ukubwa wake hatuwezi kuruhusu vyombo ambavyo havina usalama wa abiria kwa sababu tu usafiri ni tatizo tukasema basi nendeni.

Mhe. Spika, karibu siku ya tano leo hakuna safari za Unguja na Pemba kwa boti kwa sababu gani? Kwa sababu bahari ni chafu kila meli inafika Nungwi inarudishwa na mawimbi. Meli ya MV. Maendeleo imeanza safari zake kuanzia jana na itafanya safari zake za Unguja na Pemba kila baada ya siku 2 inakwenda leo iko kule, leo inarudi na kesho inakwenda tena. Mhe. Spika, pia tunaandaa utaratibu angalau wiki moja kwenda Tanga kwa hivyo wale watu watakaokwenda Tanga kutoka Pemba wakusanye mizigo yao kila wiki tunapanga meli ya MV. Maendeleo iendezake Tanga ikifika huko Tanga sio mbali inarudi Pemba inachukua abiria inakuja Unguja. Hii nasema ni *temporary nature* lakini tunaangalia utaratibu mzuri tu wa kuwa na usafiri wa uhakika baina ya Tanga na Pemba.

Mhe. Spika, suala moja la mwisho kuhusu *safety officer* tangu tulipotoa taarifa ile hadi leo ni wangapi wameongezwa wajumbe wanataka kujua. Mhe. Spika, Bodi ya Wakurugenzi ya *ZMA* ina wataalamu wanne wa mambo ya *maritime*, tumekubaliana kwamba *structure* iliyokuwepo muundo wa *ZMA* ubadilishwe na muundo wa *ZMA* unabadilishwa na karibu sana tutakuwa na muundo ambao ni *standard* na muundo huo ndio ambao utatuwekea safi. Kwa hivyo, suala jengine ni baada ya muundo huo sasa hivi tutatumia muundo huu ambao upo

baada ya muundo huu ambao naamini ni mzuri zaidi. Matatizo haya ya *safety officers, registration*, kanuni hizi vile vile zitakuwa hazina tatizo.

Mhe. Spika, nawashukuru sana Wajumbe kwa masuala yao muhimu sana ya kujenga lakini narudia tena serikali, wizara hata siku moja haitathubutu kumdharau Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi. Na Mhe. Hamza nakuomba tena suala la kudharau hapa halipo kabisa ni kwamba tunafanya kazi na si mambo ya kufumba na kufumbua mengine yanachukua siku tatu, jengine miezi mitatu, mengine miaka mitatu na mengine zaidi ya hapo. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Nakushukuru Mhe. Waziri, Mhe. Naibu Waziri pamoja na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais ambaye amepata dharura sasa hivi yeye amekwenda kwenye shughuli nyengine baada ya kupata msiba punde tu hivi. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo tunategemewa sasa tuipokee hii ripoti niwaulize basi wale wanaopokea ripoti hiyo wanyanyue mikono…

TAARIFA

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, wakati Mhe. Omar Ali Shehe akichangia alizungumza juu ya uamuzi wa serikali kuzuia Shirika la Meli ambalo alisema pale Alhaji Mzee wetu alikuwa kwenye kiti. Lakini wakati Mheshimiwa anachangia alieleza faida ya subra, na faida ya subra imeweza kupata kampuni moja kubwa sana ya Yussuf ambayo ni maarufu kujenga meli duniani.

Mimi napata tabu moja naomba muongozo wako, mimi amenitaja na waziri ameelezea maelezo ya serikali ambayo mimi kama Mwenyekiti sijapata barua inayosema serikali imekataa, na ule mchakato ulipata idhini ya serikali na Waziri wa Mawasiliano Mhe. Machano Othman Said alimkabidhi Rais wa Zanzibar ile ripoti, na Mshauri Mkuu wa Shirika la Meli alikuwa ni Ndugu Abdulhakim huyu juzi alikuwa ni Mwenyekiti jaji.

Mhe. Spika, mimi hapa napata faraja moja Mhe. Mwanasheria Mkuu alisema sio uzuri Wajumbe wa Baraza na mimi naunga mkono kuwa wenyeviti katika Mashirika ya Umma, katika Mabodi hasa ya Biashaara kwa sababu kuna *conflict of interest*. Lakini sijui mwongozo wako Mhe. Spika, naweza kutoa maelezo kwa sababu nimetajwa si kwa vibaya au tuache hivi hivi tu siku nyengine kwa sababu ninayo maelezo ambayo ya ushahidi wa serikali ilisema nini. Serikali haijasema hapana tunakataa deni kubwa, kwa hiyo nimeona mheshimiwa unipe muongozo wako.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe muongozo wa Spika unahitajika juu ya suala hili, lakini ningependa nikaelewa muda kwa kweli mfupi sana kuweza kueleza jambo hilo leo. Lakini ningependa kuelewa kama kuna jambo lolote kutokana na maelezo ya Mhe. Omar Ali Shehe ambayo yako kinyume na mtazamo ule wa serikali kiasi cha kwamba sasa yapate ufafanuzi zaidi ambao wewe kama Mwenyekiti wa Bodi wakati huo Shirika la Meli ungeweza kuyatoa. Sina hakika juu ya hilo na bahati mbaya, hiyo ndio nilikuwa najaribu kuangalia katika maelezo yake kuna kitu gani ambacho kilikuwa kimekwenda kinyume na hali halisi ya suala la Shirika la Meli. Labda tukielewa hivyo lakini muda wenyewe ni mfupi mno kwa sababu tuna dakika kama 7 tu pale, nadhani suala hili kwa wakati huu hatuwezi tukalitoa lakini angalau basi nipate maelezo hata kama kesho juu ya hili.

Kama kuna jambo lolote ambalo limekwenda kinyume na maelezo ya Mhe. Omar dhidi ya mambo halisi yalivyokuwa katika Bodi ambayo wewe ulikuwa unaiongoza katika Shirika la Meli basi tunaweza tukaipatia nafasi. Lakini hilo sina hakika kwa hiyo naomba Waheshimiwa Wajumbe tukubali kwamba kwa muda ulivyo hapa basi suala hili tulitizame kesho nikieleweshwa zaidi juu ya hili tatizo kiasi cha kwamba Mhe. Mjumbe alazimike kutoa taarifa ya ufafanuzi wa hali halisi ambayo ameomba. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe hilo tulifanye kesho, lakini kwa kuzingatia je, una jambo gani ambalo limekwenda kinyume na hali halisi ya mambo yaliyokuwa yanafanywa na bodi uliokuwa Mhe. Mjumbe anaiongoza. Naomba nielekeze hivyo.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo basi ripoti hii ipokelewe nione wale wanaopokea ripoti hiyo wanyanyue mikono, wanaokataa ripoti. Ripoti imepokelewa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Waheshimwa Wajumbe nichukue nafasi tena kwa kushirikiana vya kutosha kuendesha shughuli zetu hizi. Tunakumbushwa kwamba tuna kiporo cha semina pale Zanzibar Beach kwa hiyo naahirisha kikao hiki hadi kesho tarehe 27/01/2012 saa 3:00 asubuhi.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa
hadi tarehe 27/01/2012 saa 3:00 asubuhi)